



AFYA

Wizara ya Afya yaanza mpito hadi mfumo mpya wa afya wa kidijitali wa SHA **UK 12**



UHIFADHI

Jamii za wafugaji zapokea Sh655m kutokana na mapato ya kaboni

UK 22

Julai 7, 2026

www.gaa.go.ke
My

TATHMINI YAKO YA WIKI
Gov.

TOLEO La. 1/2026-2027

Ujenzi wa upanuzi wa SGR hadi Malaba waanza

Kandarasi ya Sh 700 bilioni ya ujenzi wa awamu ya upanuzi huo ilitolewa kwa kampuni za China, China Communications Construction Company (CCCC) na China Road and Bridge Corporation (CRBC), ambazo zote zimewahi kutekeleza miradi mikubwa ya miundombinu nchini Kenya. Ushiriki wa kampuni hizo unaashiria dhamira ya serikali ya kuhakikisha mradi huo unatekelezwa kwa kuzingatia viwango vya kimataifa vya ubora na ufanisi.

HABARI KAMILI UK 2



Find us also on;



Government Advertising Agency



@MyGovKe



@GAA_Kenya



<https://gaa.go.ke>

Contacts: mygovads@gaa.go.ke | editorial@gaa.go.ke | director@gaa.go.ke | (+254) 020 4920000/1



Ujenzi wa upanuzi wa reli ya kisasa (SGR) hadi Malaba waanza

NA EMILY KADZO NA HILLARY SHIMNAGHA (KNA)

Ujenzi uliokuwa ukisubiriwa kwa muda mrefu wa awamu ya upanuzi wa Reli ya Kisasa ya Standard Gauge Railway (SGR) kutoka Naivasha hadi Kisumu na Malaba umeanza rasmi katika Kaunti ya Narok, hatua muhimu katika mpango kabambe wa Kenya wa kuboresha miundombinu ya usafiri na kuimarisha biashara ya kikanda. Mkataba wa ujenzi wa reli hiyo wenye thamani ya Shilingi bilioni 700 ulitolewa kwa kampuni za China Communications Construction Company (CCCC) na China Road and Bridge Corporation (CRBC), ambazo tayari zimetokeleza miradi mikubwa ya miundombinu nchini Kenya. Ushiriki wa kampuni hizo unaonyesha dhamira ya serikali ya kuhakikisha mradi huo unatekelezwa kwa viwango vya kimataifa vya ubora na ufanisi. Serehe ya uzinduzi wa ujenzi huo ilihudhuriwa na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Kenya (Kenya Railways), Philip Mainga, Kamishna wa Kaunti ya Narok Kipkech Lotiatia, Katibu wa Kaunti Mayian Tuya,



Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli la Kenya, Philip Mainga (katikati), akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi rasmi wa upanuzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kutoka Naivasha hadi Kisumu na Malaba, katika kaunti ya Narok. Mradi huo unatarajiwa kuimarisha usafirishaji kati ya Bandari ya Mombasa na mpaka wa Uganda. PICHA: HILLARY SHIMNAGHA/KNA.

maafisa wa serikali ya kitaifa, wawakilishi wa Tume ya Kitaifa ya Ardhi (NLC), wakandarasi wa mradi huo, viongozi wa eneo hilo pamoja na wadau wa jamii. Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mainga alisema kuwa upanuzi wa reli ya SGR unatarajiwa kuboresha ufanisi wa usafirishaji kati ya Bandari ya

Mombasa na mpaka wa Uganda. Alisema reli hiyo ni sehemu ya mpango mpana wa serikali wa kupanua SGR kutoka Naivasha hadi Kisumu na baadaye Malaba, hatua itakayorahisisha usafirishaji wa mizigo na kuongeza ufanisi wa usafiri katika Ukanda wa Kaskazini (Northern Corridor). Mbali na usafirishaji wa mizigo,

Mainga alisema mradi huo unatarajiwa kuchochea uchumi wa maeneo mbalimbali, kuunda nafasi za ajira na kuvutia uwekezaji mpya katika sekta za kilimo, viwanda na utalii. “Upanuzi wa SGR kutoka Naivasha hadi Kisumu na Malaba ni zaidi ya reli; ni ishara ya dhamira ya Kenya katika kuimarisha ushirikiano wa kikanda, mageuzi ya kiu-chumi na maendeleo endelevu.” “Ukikamilika, mradi huu hautarahisisha tu usafirishaji wa mizigo bali pia utaimarisha nafasi ya Kenya kama lango kuu la Afrika Mashariki,” alisema Mainga. Aliongeza kuwa mradi huo utazalisha maelfu ya nafasi za ajira wakati wa ujenzi na kuleta manufaa ya muda mrefu kwa uchumi kupitia kuboreshwa kwa huduma za usafirishaji, kuimarishwa kwa muun-

ganiko wa kikanda na ufanisi wa usafirishaji wa mizigo. “Kaunti ya Narok, ambayo inapitiwa na takriban kilomita 100 za mkondo wa SGR, ina nafasi muhimu katika mradi huu wa mageuzi ya miundombinu. Wananchi wa Narok wameonyesha ari na matumaini makubwa kutokana na fursa nyingi zinazotarajiwa kufunguliwa na mradi huu,” alisema Mainga. Aliwataka wamiliki wa ardhi na watu wote watakoathiriwa na mradi huo kushirikiana na mashirika ya serikali wakati wa mchakato wa ununuzi wa ardhi, akiwahakikishia kuwa tathmini na fidia zitatekelezwa kwa uwazi kwa mujibu wa Sheria ya Ardhi ya mwaka 2012. Mainga aliwahimiza wakazi kuwasiliana moja kwa moja na Tume ya Kitaifa ya Ardhi (NLC) ili kuhakikisha malalamiko na masuala yao yanashughulikiwa kwa haki. Kuanza kwa ujenzi huo kunafuatia tangazo la Shirika la Reli Kenya kwamba mchakato wa upatikanaji wa ardhi kwa ajili ya kituo kipya cha SGR cha Kisumu unaendelea vizuri.

ENDELEA UK 3

“Ukikamilika, itarahisisha sio tu usafirishaji wa mizigo bali pia itaainisha upya nafasi ya Kenya kama lango la kuingia Afrika Mashariki.”



BIOVAX
Protecting Health. Promoting Life

KENYA BIOVAX INSTITUTE LIMITED

NATIONAL TENDER

TENDER REF NO.	BIOVAX/PREQ/2026-2027-2028-2029
TENDER NAME:	REGISTRATION OF CONTRACTORS/SUPPLIERS/SERVICE PROVIDERS FOR THE FINANCIAL YEARS 2026-2027-2028-2029

- 1.1 The Kenya BioVax Institute Limited invites eligible candidates to apply for consideration to be included in our List of Registered contractors/suppliers/service providers.

TENDER NUMBER	TENDER NAME	CATEGORY	CLOSING DATE
BIOVAX/PREQ/2026-2027-2028-2029	REGISTRATION OF CONTRACTORS/SUPPLIERS/SERVICE PROVIDERS FOR THE FINANCIAL YEARS 2026-2027-2028-2029	BIDDERS TO CHOOSE FROM THE LIST PROVIDED IN THE TENDER DOCUMENT	27th July 2026 at 11.00 am

- 1.2 Interested eligible candidates may obtain further information and inspect the prequalification tender document from Kenya BioVax Institute's website (www.biovax.go.ke).
- 1.3 A complete set of prequalification tender document may be obtained by interested candidates through the menu **Opportunities** then **Suppliers Registration Portal** and filled online via the link <https://suppliers.biovax.go.ke:4411/>.
- 1.4 Candidates will be required to register and upload valid mandatory documents and proof of qualification via the **Suppliers' Registration link** (<https://suppliers.biovax.go.ke:4411/>).
- 1.5 **Candidates are allowed to choose various categories in which they deem suitable to participate in.**
- 1.6 Any requests for clarifications can be sent to the email address procurement@biovax.go.ke.
- 1.7 Late bids will be received but not included in the initial List of Registered Suppliers. The same will be evaluated and considered within **six (6) months**.

MANAGER, SUPPLY CHAIN MANAGEMENT,
KENYA BIOVAX INSTITUTE LIMITED



MINISTRY OF LABOUR AND SOCIAL PROTECTION

STATE DEPARTMENT FOR LABOUR AND SKILLS DEVELOPMENT

DIRECTORATE OF OCCUPATIONAL SAFETY AND HEALTH SERVICES

INVITATION OF APPLICATIONS FOR APPROVAL TO SERVE AS COMPETENT PERSONS AND INSTITUTIONS UNDER THE OCCUPATIONAL SAFETY AND HEALTH ACT, 2007

Applications are invited from qualified persons and institutions interested in serving under the provisions of the Occupational Safety and Health Act, 2007 on behalf of the Directorate of Occupational Safety and Health Services in the following categories:

- First Aid Auditors**
- Training Institutions for Working at Height**

Details about minimum qualifications and application can be accessed from:

<https://doshmis.go.ke> or www.labour.go.ke or obtained from the Directorate of Occupational Safety and Health Services, Safety House, Commercial Street, Industrial Area, 4th floor Room 412, Nairobi or in all our 51 offices Country wide.

Applicants are requested to lodge their applications online, by **1st August 2026**, and attach certified copies of certificates, testimonials, CVs and make a payment of non-refundable application fee of KSh.2,000.

For any further inquiries contact the office through the e-mail addresses: info@doshmis.go.ke or doshdept@labour.go.ke

Only those who qualify will be contacted.

Dr. Musa Nyandusi, OGW
Secretary of Occupational Safety and Health



ENDELEA KUTOKA UK 2

Timu ya wataalamu kutoka sekta mbalimbali, kwa ushirikiano na NLC, inaendelea na uhakiki wa maeneo husika ili kuhakikisha mashamba na mali zote zitakazoathiriwa zinatambuliwa kwa usahihi. "Utaratibu huu wa kina unaonyesha dhamira yetu ya kutekeleza mradi huu kwa uwajibikaji kwa kuzingatia uwiano kati ya utekelezaji wa haraka wa miundombinu na kulinda haki na maslahi ya kila mtu atakayeathiriwa," alieleza Mainga. Alisisitiza kuwa uwazi na haki ni misingi muhimu ya mchakato huo, akiongeza kuwa Shirika la Reli Kenya limejitolea kulinda maslahi ya jamii. Kwa mujibu wa Wizara ya Barabara na Uchukuzi, mradi wa upanuzi wa reli hiyo utatekelezwa katika awamu mbili. Awamu ya 2B itahusisha ujenzi wa reli yenye urefu wa takriban kilomita 264 kutoka Naivasha hadi Kisumu, ikijumuisha tawi la kilomita 8.9 litakalounganisha reli hiyo na Bandari ya Kisumu. Awamu ya 2C itaunganisha reli kutoka Kisumu hadi Malaba, hivyo kuunganisha mtandao wa reli wa Kenya na Uganda na kuimarisha ushirikiano wa kikanda siku zijazo. Reli hiyo mpya itapitia kaunti za Narok, Bomet, Kericho, Nyamira na Kisumu kabla ya kufika Malaba kwenye mpaka wa Kenya na Uganda.

Daraja la juu la Barabara ya Ngong laleta afueni kwa madereva Nairobi

NA NELLY KOSGEY (PCO)

Rais William Ruto ameizindua rasmi barabara ya juu (Flyover) ya Ngong Road–Naivasha Road yenye thamani ya Shilingi bilioni 3.8, hatua inayoweza alama muhimu katika juhudi za kuboresha mfumo wa usafiri wa Jiji la Nairobi. Barabara hiyo ya juu yenye urefu wa mita 820, iliyotekelezwa na Mamlaka ya Barabara za Mijini Kenya (KURA), imejengwa ili kuondoa moja ya maeneo yaliyokuwa yakisababisha msongamano mkubwa wa magari jijini, na hivyo kuboresha usafirishaji wa watu na bidhaa katika mojawapo ya njia zenye shughuli nyingi zaidi za usafiri jijini Nairobi. Mradi huo unatarajiwa kupunguza msongamano wa magari kwa hadi asilimia 60, jambo litakalopunguza kwa kiasi kikubwa muda wa safari, gharama za usafiri na kuboresha usalama barabarani. Kwa miaka mingi, madereva wamekuwa wakikumbwa na ucheleweshaji mkubwa katika eneo hilo, lakini barabara hiyo mpya ya juu inatarajiwa kutoa afueni kwa kupunguza msongamano na



Rais William Ruto (akikata utepe) anazindua daraja la juu la Barabara ya Ngong-Barabara ya Naivasha lenye thamani ya Sh3.8b jijini Nairobi.

kuboresha mtiririko wa magari. Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Rais Ruto alisisitiza tena dhamira ya Serikali ya kuendelea kuwekeza katika miundombinu ya usafiri inayochochea ukuaji wa uchumi na kuboresha maisha ya wananchi. "Uzinduzi wa barabara ya juu ya Ngong Road–Naivasha Road ni sehemu ya mpango mpana wa kupunguza msongamano wa magari jijini Nairobi, kuboresha muunganiko wa barabara na kujenga mji mkuu wa kisasa unaoweza kuhudumu ipasavyo kama lango la Afrika

Mashariki," alisema Rais Ruto. Rais alisema kuwa barabara hiyo ni sehemu ya mpango mpana wa kuboresha usafiri wa mijini unaoendelea kutekelezwa kote Nairobi. Miongoni mwa miradi mikubwa inayoendelea ni barabara ya juu ya Upper Hill–Kenyatta Avenue yenye thamani ya Shilingi bilioni 3, ambayo kwa sasa imekamili kwa asilimia 60. Miradi mingine muhimu ni pamoja na ujenzi wa barabara za kuelekea Talanta Sports City yenye thamani ya Shilingi bilioni 3.9 na uboreshaji wa State House

Road yenye gharama ya Shilingi bilioni 1.6. Aidha, maandalizi yanaendelea kwa ajili ya upanuzi wa Barabara ya Kiambu yenye urefu wa kilomita 23.5 kuwa njia mbili kwa kila upande, mradi wenye thamani ya dola za Marekani milioni 231 (takriban Shilingi bilioni 30), unaolenga kuongeza uwezo wa barabara hiyo na kuboresha mtiririko wa magari katika mojawapo ya njia zenye shughuli nyingi zaidi jijini. Sambamba na upanuzi huo wa miundombinu, Serikali imeanza kutekeleza Mfumo wa Kisasa wa Usimamizi wa Usafiri (Intelligent Transport System - ITS) utakaohusisha zaidi ya makutano 210 yenye taa za kuongozea magari kote Nairobi. Mpango huo wa awamu tatu unaokadiriwa kugharimu Shilingi bilioni 45 utawezesha usimamizi wa trafiki kwa wakati halisi, kuratibu mtiririko wa magari, kuboresha usalama barabarani na kupunguza ucheleweshaji. "Tunashughulikia kwa utaratibu changamoto za usafiri ambazo zimekwamisha ukuaji wa Nairobi kwa miongo kadhaa. Uwekezaji huu utaliweka jiji letu katika nafasi ya kuwa mji mkuu wa kisasa, wenye ufanisi na unaoweza kushindana kimataifa," alisema Rais Ruto.



ANTI-FEMALE GENITAL MUTILATION BOARD

A Society free from female genital mutilation



KENYA RAILWAYS SRBS
SOUTHWING, BLOCK "D"
2ND FLOOR
P.O. BOX 54760 - 00200
NAIROBI

Email: admin@antifgmboard.go.ke
Email: ceoantifgmboard@gmail.com

JOB OPPORTUNITIES

The Anti-Female Genital Mutilation Board is a State Corporation under the Ministry of Gender, Culture and Children Services responsible for implementing the Prohibition of Female Genital Mutilation Act, 2011. The Board invites applications from qualified persons to fill the vacancies listed below.

S/NO.	POST	GRADE	VACANCY NO.	NO OF POSTS
1.	Chief Executive Officer	AFGM 1	AFGM/1/2026	1
2.	Deputy Director, HRM & Administration	AFGM 3	AFGM/2/2026	1
3.	Accountant	AFGM 7	AFGM/3/2026	1
	TOTAL			3

For detailed job requirements visit the Anti-FGM Board's website www.antifgmboard.go.ke

Application Procedure

Qualified and interested applicants who meet the requirements should visit the Board's career page on the website. The applicants shall apply through the Anti-FGM Board's recruitment portal which is accessible through <https://jobs.antifgmboard.go.ke/>

Applications should be submitted in Pdf format not later than **5:00PM Tuesday, July 21st, 2026. (East African Time)**

No hand delivery applications shall be accepted.

"Anti-FGM Board is an equal opportunity employer".

"Any form of canvassing will lead to automatic disqualification".



KENYA REVENUE AUTHORITY
Tulipe Ushuru, Tujitegemeel

Public Notice

Removal of Excise Duty on Bottled Water

Kenya Revenue Authority notifies all licensed manufacturers and importers of bottled water and the general public that pursuant to the Finance Act, 2026 (amending the First Schedule to the Excise Duty Act, Cap 472), excise duty on bottled water is removed with effect from **1st July, 2026**. Bottled water manufactured or imported on or after this date will not be subject to excise duty and will not require to be affixed with excise stamps.

The Commissioner will issue detailed guidelines on the return of unutilized stamps and the decommissioning of digital stamps, which will be published on the official KRA website.

Manufacturers are reminded of their obligation to submit their Excise Duty Returns for the month of June 2026 and pay the taxes due by 20th July, 2026.

For further information/clarification, please call our Enforcement Division on:

Telephone No: 0709012799/0709012769/0709012318 or Email: exciselicensing@kra.go.ke

Commissioner for Micro & Small Taxpayers

www.kra.go.ke

Disclaimer: KRA notifies taxpayers that it will not accept responsibility for payments not received, credited and validated in the relevant KRA accounts.
Corruption Reporting: +254 (0726) 984 668, Email: corruptionreporting@kra.go.ke, Complaints & Information Centre Hotlines: +254 709 017 700 / 800 Email: cic@kra.go.ke



Wakulima 9,300 kupata mikopo nafuu Kirinyaga ikitoa Sh20m kwa Sacco



Gavana wa Kaunti ya Kirinyaga Anne Waiguru, pamoja na viongozi wa vikundi vya jamii na viongozi wengine wa Kirinyaga, waonyesha mfano wa hundi wakati wa utoaji wa fedha za uwezesaji kwa Saccos za mashinani.

NA DAVID WANDETO
(KNA)

Zaidi ya wakulima 9,300 katika Kaunti ya Kirinyaga wanatarajiwa kunufaika na upatikanaji bora wa mikopo nafuu baada ya serikali ya kaunti kutoa Shilingi milioni 20 kwa Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (SACCO) 20 vya ngazi ya kata, ikiwa ni sehemu ya mpango mpana wa kuwawezesha kiuchumi wakulima, vijana, wanawake na makundi yaliyo

katika mazingira magumu. Akizungumza wakati wa hafla ya ugawaji wa fedha hizo katika eneo la Kabare, Gavana wa Kaunti ya Kirinyaga, Anne Waiguru, alisema kila moja ya kata 20 za kaunti hiyo imepokea Shilingi milioni moja ili kuimarisha SACCO zinazomilikiwa na wakulima na kupanua huduma za kifedha zitakazowawezesha wanachama kuwekeza katika kilimo na shughuli nyingine za kuzalisha kipato. Gavana huyo alisema mpango huo utanufaisha moja kwa moja

wakulima 9,312 kwa kuboresha upatikanaji wa mikopo nafuu, kuhamasisha utamaduni wa kuweka akiba na kuimarisha uwekezaji katika mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo. Waiguru alisema serikali ya kaunti imejizatiti kuwawezesha wakazi kiuchumi kwa kuwekeza katika miradi iliyobainishwa kupitia ushiriki wa wananchi, akibainisha kuwa upatikanaji wa fedha za gharama nafuu bado ni mojawapo ya changamoto kubwa zinazowakabili

wakulima wadogo na wajasiriamali wa biashara za kilimo. Alisema fedha hizo zitaziwezesha SACCO kungeza utoaji wa mikopo kwa wanachama wake, kusaidia uzalishaji wa

Kuwezesha makundi kupitia vifaa vya kuzalisha kipato kunawawezesha wanufaika kuanzisha biashara endelevu.

kilimo, kuhamasisha uongezaji thamani wa bidhaa na kuboresha upatikanaji wa masoko, hatua ambayo itaongeza kipato cha kaya na kuunda nafasi zaidi za ajira. Mbali na msaada huo wa kifedha kwa SACCO, serikali ya kaunti pia ilisambaza vifaa mbalimbali vya kuwawezesha wananchi kwa vikundi vya kijamii na kaya zilizo katika mazingira magumu katika kata 16. Vifaa vilivyosambazwa vilijumuisha viti vya magurudumu kwa watu wanaoishi na ulemavu, pikipiki, vifaa vya upishi na huduma za chakula, mahema na viti, mifumo ya anwani za umma (PA), matangi ya kuhifadhi maji, majiko banifu ya kuokoa nishati, makoti ya kuakisi mwanga kwa vikundi vya wændesha bodaboda, taulo za usafi kwa wasichana, mikokoteni ya kuuzia soseji na mayai pamoja na mashine ya kuosha magari kwa kikundi cha vijana. Kwa mujibu wa Gavana huyo, vifaa hivyo viligawiwa kulingana na maombi yaliyowasilishwa na wananchi kupitia Wajumbe wao wa Bunge la Kaunti (MCA), kwa lengo la kuhamasisha kujajiri, kuboresha huduma za jamii na kuongeza kipato cha kaya. Alisema kuwawezesha vikundi vilivyojipanga kwa kuvipatia vifaa vya kuzalisha kipato kunawapa wanufaika uwezo wa kuanzisha biashara endelevu huku kukipunguza ukosefu wa ajira na utegemezi. Mwakilishi wa Wadi ya Kabare, Isaiah Mbogo alisema uwekezaji wa serikali ya kaunti katika kuwawezesha wananchi mashinani umeimarisha maisha ya wakazi na kuharakisha maendeleo katika wadi hiyo.



CHEMUSUSU WATER COMPANY LTD

ELDAMA RAVINE OFFICE, KAMELILLO ALONG RAVINE /NAKURU ROAD.

P.O. BOX 826-20103
ELDAMA RAVINE.

Email: info@chewasco.co.ke, erawasco2007@yahoo.co.uk, chewasco2015@yahoo.com
Website: www.chewasco.co.ke for free Tel: 0794 257 299



REGISTRATION OF SUPPLIERS NOTICE

CHEWASCO/REG/011/2026-2028

Chemususu Water Company limited invites interested eligible bidders for registration of suppliers for various goods, works and services for the financial year 2026/2028

A set of registration documents can be obtained by downloading from CHEWASCO Website: <https://chewasco.co.ke/tenders/> Or Public Procurement Information Portal Website: www.tenders.go.ke for free

Completed tender documents should be serialized and be enclosed in plain sealed envelopes marked with tender reference number and be addressed to: -

The Managing Director,
Chemususu Water Company Limited
P.O.Box 826-20103, ELDAMA RAVINE.
Not later than Monday 20th July 2026 at 11.30am Kenyan time
(NB: -Should be one (1) separate document for each category)

Should be deposited in the Tender Box at head office Chemususu Water Company Limited, Kamelillo offices so as to be received on/before Monday 20th July 2026 at 11.30am. The bids documents will be opened thereafter. Tenderers or their representatives are free to attend.



MERU WATER AND SEWERAGE SERVICES COMPANY LTD (MEWASSCO)

P.O BOX 859 - 60200 - MERU
Tel: 064-3132591, 0717527707
email: meruwat@gmail.com
Website: www.mewass.or.ke



REGISTRATION OF SUPPLIERS NOTICE

Meru Water and Sewerage Services Company Limited invites interested eligible bidders for registration of suppliers for various goods, works and services for Financial Years 2026/2027 and 2027/2028.

A set of the registration documents can be obtained by downloading from MEWASSCO website www.mewass.or.ke or Public Procurement Information Portal website www.tenders.go.ke for free.

Application clearly marked the Tender Number and Tender Name on a sealed envelope should be addressed to:

The MANAGING DIRECTOR,
Meru Water and Sewerage Services Co .Ltd
P.O. Box 859 - 60200
Tel 064-3132591/0717527707
MERU

Should be deposited in the tender box at the Head Office reception so as to be received on/before Friday 17th July 2026 at 10.00 am. The bid documents will be opened thereafter. Tenderers or their representatives are free to attend.

Kilifi yavutia uwekezaji wa Sh9b, yaunda ajira 14,000

NA EMMANUEL MASHA (KNA)

Kaunti ya Kilifi imevutia uwekezaji wa shilingi bilioni 9 katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, huku kampuni 14 za Maeneo ya Uzalishaji kwa Ajili ya Mauzo ya Nje (EPZ) zikizianzisha shughuli zake na kuunda zaidi ya nafasi 14,000 za ajira, Katibu Mkuu wa Idara ya Kukuza Uwekezaji, Abubakar Hassan, ametangaza. Akizungumza wakati wa uzinduzi wa Kiwanda cha Kusindika Matunda cha Milly katika Wadi ya Sabaki, Eneo Bunge la Magarini, Abubakar alisema Kilifi inaongoza kaunti nyingine za Pwani katika ukuaji wa viwanda kupitia mpango wa EPZ.

Alieleza kuwa ushirikiano kati ya Rais William Ruto na Gavana wa Kilifi Gideon Maitha Mung'aro umechangia kwa kiasi kikubwa mafanikio hayo, akibainisha kuwa idadi ya kampuni za EPZ katika kaunti hiyo imeongezeka kutoka 10 hadi 24 tangu walipoingia madarakani. Alisema mpango wa EPZ ulioanzishwa nchini Kenya miaka ya 1990 ulikuwa umekwama kwa zaidi ya miongo mitatu katika Kaunti ya Kilifi, huku kampuni 10 pekee zikiendesha shughuli zake na kuajiri takriban watu 10,000. "Hata hivyo, katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, kampuni mpya 14 zimewekeza shilingi bilioni 9 na kuunda nafasi nyingine 14,000 za ajira katika kaunti hii—idadi inayozidi



Katibu wa Kukuza Uwekezaji, Abubakar Hassan Abubakar, anazungumza na waandishi wa habari baada ya uzinduzi rasmi wa Kiwanda cha Kusindika Matunda cha Milly katika Kata ya Sabaki, Jimbo la Uchaguzi la Magarini, Kaunti ya Kilifi. Akiwa pamoja naye ni Gavana wa Kaunti ya Kilifi, Gideon Mung'aro.

jumla ya ajira zilizoundwa katika kipindi cha miaka 30 iliyotanguka," alisema Bw. Abubakar. Alisema takwimu zinaonyesha kuwa Kaunti ya Kilifi inaongoza miongoni mwa kaunti za Pwani katika uwekezaji wa EPZ, hali aliyoihusisha na mazingira

Katika kipindi cha miaka mitatu iliyopita, kampuni mpya 14 zimewekeza Shilingi bilioni 9 na kuunda nafasi mpya za ajira

mazuri ya biashara yaliyowekwa na Serikali ya Kitaifa pamoja na utawala wa Kaunti ya Kilifi. Hatua ya hivi karibuni katika safari ya Kilifi kuelekea maeendeleo ya viwanda ni uzinduzi wa kiwanda cha kusindika matunda cha Milly Fruits EPZ Ltd chenye thamani ya shilingi milioni 343, ambacho kinatarajiwa kuongeza uwezo wa kusindika matunda hapa nchini, kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno na kupanua fursa za masoko ya mazao ya Kenya katika masoko ya kikanda na kimataifa. Uwekezaji huo umewezekeza kupitia Mpango wa Maendeleo Endelevu ya Uchumi wa Miji (Sustainable Urban Economic Development - SUED) unaofadhiliwa na Serikali ya Uingereza na kutekelezwa na Financial Sector Deepening (FSD) Kenya, ambao ulitoa ufadhili wa awali wa shilingi milioni 83.8 ili kukamilisha uwekezaji wa shilingi milioni 259 uliowekwa na Milly Fruits.

Serikali kuunganisha wachezaji na timu za kimataifa za michezo

NA DICKSON MWITI (KNA)

Serikali, kupitia Idara ya Wakenya Wanaoishi Ughaibuni, inachunguza njia za kuunganisha wanamichezo vijana wenye vipaji nchini Kenya na fursa za kujiunga na timu za kulipwa nje ya nchi. Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mashindano ya kwanza ya Soka ya Kazi Majuu katika Shule ya Msingi ya Mitoone, Eneo Bunge la Buuri, Katibu Mkuu wa Idara ya Masuala ya Wakenya Wanaoishi Ughaibuni, Roseline Njogu, alisema mazungumzo yako katika hatua za mwisho kuhusu kuanzisha mifumo itakayowawezesha wanamichezo wenye vipaji katika soka, riadha, mpira wa wavu na michezo mingine kupata fursa nje ya nchi. "Kama mnavoyjua, michezo ni sehemu muhimu ya taifa hili. Tunajulikana duniani kwa mafanikio yetu katika riadha pamoja na vipaji vingine, na tunaunda fursa zitakazowaunganisha vijana na timu za nje ya nchi. Hii ni sehemu ya kazi tunayoifanya kama idara," alisema Njogu. Alisema mpango huo unalenga kuwasaidia vijana kutambua kuwa, ingawa vipaji vyao vinakuzwa hapa nchini, vinaweza kuwafungulia milango ya fursa katika medani ya michezo duniani.



Kutoka Kushoto: Mbunge wa Buuri Rindikiiri Mugambi, Katibu wa Misitu Mugambi Gitonga, Katibu Mkuu wa Masuala ya Diaspora Roseline Njogu wakati wa uzinduzi wa mashindano hayo.

Zaidi ya vijana 2,000 walihudhuria uzinduzi wa Mashindano ya Soka ya Kazi Majuu, ambapo tukio hilo liliwaleta pamoja vijana waliounganishwa na michezo, vipaji na imani kwamba fursa zinaweza kubadili maisha yao. Idara hiyo ilisambaza sare za soka na mipira kwa timu 60 za jamii, huku timu 10, zikiwemo timu mbili za wanawake, zikishiriki katika raundi ya ufunguzi wa mashindano hayo. Njogu alisema mashindano hayo yanahusu zaidi ya mchezo wa soka pekee, akibainisha kuwa yamebuniwa

KWA TAKWIMU

2,000

Zaidi ya vijana 2,000 walihudhuria uzinduzi wa Mashindano ya Soka ya Kazi Majuu.

kuunganisha vipaji na fursa huku yakionyesha vijana kuwa ndoto zao zinaweza kutimia hata nje ya mipaka ya Kenya. "Iwe mustakabali wao uko uwanjani, katika biashara, kazi za ufundi au katika soko la ajira la kimataifa, Kenya inaamini katika uwezo wao," alisema. Alisisitiza tena dhamira ya Serikali ya kuendelea kuwawekeza vijana fursa kupitia mpango wa Kazi Majuu na akawasilisha ujumbe wa Rais William Ruto wa kuwaunga mkono vijana wanaotafuta ajira na kujenga taaluma zao ndani na nje ya nchi. Washiriki pia walipatiwa elimu kuhusu fursa zinazopatikana kupitia mpango wa Kazi Majuu na kuelimishwa kuhusu uhamiaji salama wa wafanyakazi kupitia mashirika ya uajiri yaliyo-sajiliwa na kupewa leseni.



MINISTRY OF MINING, BLUE ECONOMY AND MARITIME AFFAIRS

PUBLIC NOTICE

EXTENSION OF COMMENTS AND PROPOSALS SUBMISSION DATE

EXTENSION OF DATE FOR SUBMISSION OF COMMENTS ON THE DRAFT MINERALS, MINING AND VALUE ADDITION POLICY, THE DRAFT EXPLOSIVES BILL 2026 AND THE DRAFT MINING (MINE HEALTH, SAFETY AND ENVIRONMENT) REGULATIONS, 2026.

Following the issuance of the GAZETTE NOTICES (No. 8980 and No. 8981) of Friday, 12th July 2026 and the Public Notice 'CALL FOR COMMENTS AND INVITATION FOR PUBLIC PARTICIPATION ON THE DRAFT MINERALS, MINING AND VALUE ADDITION POLICY, THE DRAFT EXPLOSIVES BILL 2026 AND THE DRAFT MINING (MINE HEALTH, SAFETY AND ENVIRONMENT) REGULATIONS, 2026', published on **Tuesday, 16th June 2026**, inviting the submission of comments and proposals on the three draft instruments.

Members of the public are hereby informed of the extension of submission date to **Wednesday, 15th July 2026**, from the earlier stated date of 8th July 2026.

The Ministry will have virtual sessions on Thursday and Friday 9th July 2026 and 10th July 2026 between 10.00am – 1.00 p.m. Links will be shared on the Ministry's Website and social media pages by COB, Wednesday 8th July, 2026

To access the draft instruments and their regulatory impact statements, visit the Ministry's website at www.mining.go.ke – media centre/resources/ public notices. Written submissions should be forwarded to:

**The Principal Secretary
State Department for Mining
Ministry of Mining, Blue Economy and Maritime Affairs
P.O. Box 30009 - 00100, Nairobi
Hand-delivered to: 3rd Floor, Works Building, Ngong Road, Nairobi
Or by Email: ps@mining.go.ke**

All submissions should clearly indicate the specific Part, Chapter or Regulation to which the comment refers. Submissions should be made using the prescribed template provided below:

TEMPLATE TO SUBMIT COMMENTS

NAME OF ORGANIZATION / INDIVIDUAL PERSON				
S/No.	Part / Section	Issue of Concern	Justification	Recommendations
1				
2				

Members of the public are further informed that the **venue for the Public Participation meeting for Narok, Bomet and Kericho Counties**, scheduled for 8th July 2026, has been changed to **Neat Mara Hotel, Lolgorian Town, Narok.**

**HON. HASSAN ALI JOHO, EGH
CABINET SECRETARY
MINISTRY OF MINING, BLUE ECONOMY AND MARITIME AFFAIRS**

Serikali na mashirika ya mawasiliano zashirikiana kuboresha huduma za ICT

NA SHARON NJERU NA PASKAL OSONGA

Serikali imethibitisha upya dhamira yake ya kushirikiana na waendeshaji wa mitandao ya simu ili kuboresha ubora wa huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (ICT), ikisema kuwa mawasiliano ya kuaminika ni msingi muhimu wa ukuaji wa uchumi na upatikanaji wa huduma za umma. Akizungumza wakati wa mkutano wa wadau ulioandaliwa na Mamlaka ya Mawasiliano Kenya (CA), Katibu Mkuu wa Idara ya Utangazaji na Mawasiliano ya Simu, Stephen Isaboke, alisema kuwa serikali na kampuni za mawasiliano zilifanya kikao cha mashauriano kutathmini ubora wa huduma za mawasiliano nchini na kushughulikia changamoto zinazojitokeza huku mahitaji ya huduma za kidijitali yakiendelea kuongezeka. Alisema kuwa majadiliano yalijikita katika utayari wa mitandao kwa enzi wa Akili Bandia (AI) na



Katibu wa Utangazaji na Mawasiliano ya Simu, Stephen Isaboke (katikati), akizungumza na vyombo vya habari jijini Nairobi baada ya mazungumzo na Afisa Mkuu Mtendaji wa Safaricom, Peter Ndegwa (kushoto), na Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano ya Kenya, David Mugonyi (kulia). Mazungumzo hayo yalilenga kutathmini ubora wa huduma nchini kote na kushughulikia changamoto zinazojitokeza

teknolojia ya 5G, kupanua huduma za mawasiliano katika maeneo ambayo hayajahudumiwa ipasavyo, na kuhakikisha uwepo wa mawasiliano imara kuelekea Mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON) ya mwaka 2027, ambayo Kenya itaandaa kwa ushirikiano na mataifa mengine. "Tutafanya kila lina-lowezekana kuhakikisha kuwa Wakenya wanapata

huduma wanzostahili. Pale ambapo kuna mapungufu, hasa kadri teknolojia inavyoendelea kubadilika, tutashirikiana kuyatatua," alisema Isaboke. Katibu huyo alisema kuwa huduma bora za mawasiliano ni muhimu kwa wananchi wanaopata huduma za serikali, usajili wa wapigakura na uchaguzi ujao, akiongeza kuwa kila Mkenya anapaswa kuwa na huduma

za mtandao za kuaminika bila kujali anakoishi. Aliongeza kuwa serikali itashirikiana kwa karibu na Wizara ya Michezo pamoja na wadau wengine kuhakikisha kuna mawasiliano ya kuaminika katika viwanja vya michezo, viwanja vya ndege, hoteli na maeneo mengine yatakayosaidia

kufanikisha uandaaji wa mashindano ya AFCON. Afisa Mkuu Mtendaji wa Safaricom, Peter Ndegwa, alisema kuwa waendeshaji wa mitandao ya simu wanaendelea kujitolea kutoa huduma bora, si tu kwa kuzingatia masharti ya leseni, bali pia kukidhi matarajio ya wateja.



ADDENDUM NO. 3 OF 7TH JULY 2026

Reference is made to the publication of the National Open Tender in the Government Advertising Agency's My Gov edition of 9th June 2026 and addendum no 2 of 16th June 2026

The Procuring Entity, the National Irrigation Authority (the Authority), hereby amends the tender submission mode and submission deadline as indicated below;

S. No.	Tender No.	Initial Tender Name	Revised tender name	Initial Tender Submission Deadline	Revised Tender Submission Deadline	Target Group
1.	NIA/T/020/2025-2026	Provision of general Insurance services to National Irrigation Authority FY 2026/2027	Provision of Insurance Brokerage Services – General Insurance	As published in MyGov Edition of 9 th June 2026, Issue No. 47/2025-2026	16 th July 2026 At 12.00 Noon Local Time	General
2.	NIA/T/021/2025-2026	Provision of staff and directors' medical insurance services for FY 2026/2027	Provision of Insurance Brokerage Services – Staff and Directors Medical Insurance	As published in MyGov Edition of 9 th June 2026, Issue No. 47/2025-2026	16 th July 2026 At 12.00 Noon Local Time	General

Detailed tender documents, including the mandatory preliminary requirements and the technical and financial evaluation criteria, may be obtained free of charge by interested and eligible tenderers from the Authority's website at <http://www.irrigationauthority.go.ke/tenders> or the Public Procurement Information Portal (PIIP) at <https://tenders.go.ke> from 7th July 2026.

Any requests for clarification regarding the tender documents should be submitted in writing via email to purchasing@irrigationauthority.go.ke or ceo@irrigationauthority.go.ke within the timelines specified in the tender documents.

Any clarifications issued and/or addenda arising during the tendering process shall be published on the Authority's website and the Public Procurement Information Portal (PIIP). It is the responsibility of all prospective tenderers to regularly check these platforms for any updates before submitting their bids.

Completed tenders must be deposited in the designated Tender Box located at the **National Irrigation Authority Headquarters, Irrigation House, Lenana Road, Nairobi**, so as to be received on or before **16th July 2026 at 12.00 Noon**

Physical Address
Chief Executive Officer/CEO
National Irrigation Authority (NIA)
Unyunyizi House,
Lenana Road, Hurlingham, Nairobi, Kenya
Tel: +254-20-2711380/468
Fax: +254-20-2722821/2711347
E-mail: purchasing@irrigation.or.ke




PUBLIC NOTICE

INVITATION TO APPLICATIONS TO THE EMERGING TECHNOLOGIES REGULATORY SANDBOX

The Communications Authority of Kenya (CA) is the regulatory agency for information and communications in Kenya with responsibilities in telecommunications, cyber security, e-commerce, broadcasting and postal/courier services. The CA is also responsible for managing the country's numbering and frequency spectrum resources, administering the Universal Service Fund (USF) as well as safeguarding the interests of consumers of ICT services.

As the ICT industry regulator, the Authority is committed to fostering innovation, promoting market growth and enhancing consumer protection in Kenya's dynamic information and communications sector. In this regard, the Authority has in place an Emerging Technologies Regulatory Sandbox which provides a controlled environment for innovators to test novel digital communication products, services and business models that potentially fall outside existing regulatory frameworks.

The Emerging Technologies Regulatory Sandbox also enables collaboration between innovators and the regulator across broadcasting, cybersecurity, multimedia, telecommunications, ecommerce, postal and courier services.

CA is pleased to invite interested and eligible innovators, entrepreneurs, technology companies, and researchers to apply for admission into its Emerging Technologies Regulatory Sandbox for the Financial Year 2026/2027.

Applications are invited from diverse areas including, but not limited to Next-Generation Networks (5G/6G applications), Internet of Things (IoT) and Machine-to-Machine (M2M) communications, Over-The-Top (OTT) services and applications, digital broadcasting and content delivery innovations, cybersecurity solutions and tools, spectrum management and sharing technologies, Artificial Intelligence (AI) in information and communications and accessibility technologies for unserved and underserved populations in Kenya.

Interested innovators can submit their applications to the Emerging Technologies Regulatory Sandbox at this link: <https://sandbox.ca.go.ke/> on or before **July 30th, 2026**.

David Mugonyi, EBS
Director General/CEO

Head Office CA Centre P.O. Box 14448 Nairobi 00800 Mobile: 0703042000 Email: info@ca.go.ke	CA Western Regional Offices 15th Floor, Daima Towers, Northern Wing, Eldoret P.O. Box: 2346, Eldoret 30100 Mobile: 0703 042105 Email: wro@ca.go.ke	Coast Regional Office 3 rd Floor, NSSF Building P.O.Box 8041 Mombasa 80100 Mobile: 0703042152 Email: cro@ca.go.ke	Central Regional Office Ground Floor, Advocates Plaza P.O. Box 134 Nyeri 10100 Mobile: 0703042181 Email: cero@ca.go.ke	Nyanza Regional Office 2 nd Floor Lake Basin Mall, P.O. Box 2016 Kisumu 40100 Mobile: 0703042130 Email: nro@ca.go.ke
---	--	--	---	---

Waziri azindua vituo vitatu vya kidijitali kukuza ujuzi wa vijana Nyandarua

NA HANIFA TAMIM (PCO)

Serikali imeongeza juhudi za kupanua upatikanaji wa huduma za kidijitali na kuunda fursa kwa vijana kufuatia uzinduzi rasmi wa vituo vitatu vya kidijitali katika maeneo ya Wiyumiririe, Passenga na Mirangine, ndani ya Eneo Bunge la Ol Kalou, Kaunti ya Nyandarua. Vituo hivyo vilizinduliwa na Waziri wa Habari, Mawasiliano na Uchumi wa Kidijitali, William Kabogo, ambaye alisema kuwa

vituo hivyo vitakuwa na mchango mkubwa katika kuwapatia vijana ujuzi wa kidijitali, kuhamasisha ubunifu na kuunganisha jamii na fursa zinazojitokeza katika uchumi wa kidijitali. Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Bw. Kabogo alisema Serikali imejitolea kuhakikisha kwamba kila Mkenya, bila kujali anapoishi, anapata fursa ya kutumia teknolojia na kunufaika na mabadiliko yanayoendelea ya kidijitali nchini. "Vituo hivi vya kidijitali si



Waziri wa Habari, Mawasiliano na Uchumi wa Kidijitali, William Kabogo, akizungumza wakati wa uzinduzi wa vituo vipya vitatu vya kidijitali huko Wiyumiririe, Passenga na Mirangine katika eneo bunge la Ol Kalou, Kaunti ya Nyandarua.

majengo yaliyowekwa kompyuta na huduma za intaneti pekee. Ni vituo vya fursa ambapo vijana wanaweza kupata ujuzi wa kidijitali, kufanya ubunifu, kupata ajira za mtandaoni na kubuni suluhisho zinazoboresha maisha yao pamoja na jamii wanamoishi. Lengo letu ni kuhakikisha hakuna Mkenya anayesalia nyuma katika enzi ya kidijitali," alisema Bw. Kabogo. Vituo hivyo vitatu ni sehemu ya Mpango wa Kitaifa wa Vituo vya Kidijitali wa Serikali, unalenga kuziba pengo la kidijitali kwa kupanua upatikanaji wa intaneti ya gharama nafuu, mafunzo ya ujuzi wa kidijitali, maeneo ya ubunifu pamoja na huduma za kidijitali za Serikali. Kupitia mpango huo, maelfu ya vijana wanatarajiwa kupata ujuzi unaohitajika ili kushindana katika soko la kimataifa la kidijitali linalokua kwa kasi. Vikiwa vimeanzishwa kupitia ushirikiano kati ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Mfuko wa Maendeleo ya Maeneo Bunge (NG-CDF), vituo hivyo vitatoa huduma za matumizi ya kompyuta, intaneti ya kasi na mafunzo ya ujuzi wa kidijitali.



KENYA FOREST SERVICE



PUBLIC NOTICE

CALL FOR PUBLIC VIEWS ON PROPOSED CONSTRUCTION OF AN AIRSTRIP IN KITHOKA BEAT IN MERU FOREST STATION, MERU COUNTY

The Kenya Forest Service (KFS) proposes to construct an airstrip and ancillary infrastructure at Upper Imenti Forest (Meru Forest Station) to enhance aviation access for forest management, emergency response, and regional economic development. The Preliminary site surveys and wind assessment have found the proposed site as suitable for the proposed project. The proposed airstrip and ancillary infrastructure will occupy approximately 11 hectares. The project site is characterized by sparse vegetation cover and is therefore expected to result in minimal ecological disruption.

In compliance with the Constitution of Kenya, relevant statutory laws, regulations, and guidelines on public participation, the Kenya Forest Service invites members of the public and other stakeholders to submit their views, comments, concerns, and recommendations regarding the proposed construction of an airstrip including the runway, apron, and ancillary infrastructure.

Stakeholders are requested to submit their written views to the County Forest Conservator Office, Meru Town or download the public participation questionnaire from KFS website (www.kenyaforestservice.org) and submit to the above office or email: director@kenyaforestservice.org. Your comments and submissions will be treated with utmost confidentiality and should be received on or before **21st July, 2026**.

For further information or clarification regarding the proposed project, Please contact Kenya Forest Service through Telephone No. **+254 202502508** /or email director@kenyaforestservice.org

Chief Conservator of Forests
Karura, off Kiambu Road
P.O Box 30513- 00100
Nairobi, Kenya



OFFICE OF THE DIRECTOR OF PUBLIC PROSECUTIONS

OUR MISSION:

"To provide an impartial, effective and efficient prosecution service to all"

PUBLIC NOTICE

THE OFFICE OF THE DIRECTOR OF PUBLIC PROSECUTIONS (ODPP) INVITES INTERESTED BIDDERS FOR THE SALE OF UNSERVICEABLE MOTOR VEHICLES AND ABSOLUTE STORES ON 22/7/2026 AT 10.00 A.M. AT OUR NAIROBI OFFICES.

CONDITIONS OF SALE

1. APPOINTED AUCTIONEER – **TRENAD AUCTIONEERS.**
2. VIEWING SHALL BE FROM **9TH JULY TO 17TH JULY 2026**, DURING NORMAL WORKING HOURS, I.E. **9.00 A.M. – 4.00 P.M.** THE GOODS WILL BE OFFERED FOR SALE ON AS IS WHERE IS AS BASIS.
3. INTERESTED BIDDERS FOR MOTOR VEHICLES WILL PAY A DEPOSIT OF 10% OF THE RESERVE PRICE, AND KSHS. 5,000 FOR STORES, WHICH WILL BE SOLD AS ONE LOT. THE DEPOSIT WILL BE REFUNDED TO THE UNSUCCESSFUL BIDDERS. THE MONEY WILL BE PAID INTO THE OFFICE OF THE DIRECTOR PUBLIC PROSECUTIONS ACCOUNT.

ACCOUNT NAME: REC-DIRECTORATE OF PUBLIC PROSECUTIONS
ACCOUNT NUMBER: 1000181605
BANK: CENTRAL BANK OF KENYA
4. INTERESTED BIDDERS ARE URGED TO DOWNLOAD THE CATALOGUE CONTAINING DETAILS OF THE MOTOR VEHICLES AND ASSORTED STORES EARMARKED FOR SALE FROM THE ODPP WEBSITE WWW.ODPP.GO.KE AND PPII PORTAL INTERESTED BIDDERS ARE URGED TO VERIFY THE DETAILS OF THE MOTOR VEHICLES, AS PARTICULARS ARE NOT WARRANTED BY ODPP OR THE AUCTIONEER WHATSOEVER.
5. BIDDERS SHALL PAY **25%** OF THE SALE PRICE AT THE FALL OF THE HAMMER, AND THE BALANCE WITHIN SEVEN **(7) DAYS**. FAILURE TO WHICH THE BIDDER WILL FORFEIT THE DEPOSIT.
In line with the Government's commitment to expanding reliable electricity transmission infrastructure and enhancing access to affordable electricity, KETRACO continues to explore innovative financing mechanisms, including Public-Private Partnerships (PPPs), for the development of strategic transmission projects.

The Public Private Partnerships Act, 2021 provides for the participation of the private sector in the financing, development, operation and maintenance of public infrastructure through both competitive procurement and Privately Initiated Proposals (PIPs).

As part of its mandate and in line with the Public Private Partnerships Act, 2021, KETRACO has received Privately Initiated Proposals (PIPs) for the development of strategic electricity transmission infrastructure as set out in Table 1.

These projects form an integral part of the Transmission Master Plan 2025 - 2044 and have been considered for implementation under the PPP framework in line with national infrastructure development priorities.

2. DESCRIPTION OF THE PROPOSED PROJECTS

Project	Project Name	Objectives	Private Parties Involved	Projected Completion Timelines
1	220kV Kiambere - Rabai LILO (Mutomo)	Segment long 220kV line, improve reliability of supply and extend high voltage network to Mutomo.	Project proposal received from: 1. Pabari Investment Limited 2. ENCOMM 3. AEE Power	2029/30
	70km 132kV Mutomo-Makindu			2029/30
2	Voi 400/132kV substation and 132kV intertie to existing network	Segment long 400kV line, improve reliability of supply and reinforce 132kV system along Mombasa - Nairobi transport corridor	Project proposal received from: 1. Pabari Investment Limited 2. ENCOMM 3. AEE Power	2030/31
	110km Voi- Taveta 132kV	Extend 132kV network to Taveta and increase system reliability for load currently supplied via long 33kV lines through establishment of a new 132/33kV substation at Taveta		2030/31
3.	150km Rumuruti-Maralal 132kV	Extend 132kV network to Maralal and increase system reliability for load supplied via long 33kV lines through establishment of new 132/33kV substation at Maralal.	Project proposal received from: 1. Pabari Investment Limited 2. ENCOMM	2029/30
4	50km Sotik-Kilgoris	Extend 132kV network to Kilgoris and increase system reliability for load supplied via long 33kV lines. Establish 132/33kV substation at Kilgoris	Project proposal received from: 1. Pabari Investment Limited 2. ENCOMM	2028/29




Figure 1: Privately Initiated Proposed Transmission Projects

3. ESTIMATED PROJECT COSTS

The total project cost is estimated to be between Ksh.50 Billion and Ksh.65 Billion. These costs are preliminary and for the scope extent as shared by the proponents.

The final project cost shall be subject to:

- A transparent & competitive price discovery for the EPC costs
- detailed resettlement action plan (RAP) report as per final route alignment for the Land & ROW cost

These including any other related projects costs shall be subjected to affordability and value for money assessments at the end of the project development report (PDR) phase

The same will be tried up at financial close and only projects that meet the affordability and value for money criteria as required by the PPP Act cap 2021 shall be considered for further processing.

4. STAKEHOLDERS LIKELY TO BE AFFECTED OR IMPACTED BY THE PROJECT

1.	KETRACO staff
2.	KETRACO Board Members
3.	Project Affected Persons
4.	Local communities
5.	Host Communities
6.	National Government
7.	County Governments
8.	National Treasury
9.	Office of the Attorney General
10.	Ministry of Energy and Petroleum
11.	EPRA
12.	Kenya Power
13.	GDC
14.	KENGEN
15.	REREC
16.	NuPEA
17.	Water Resources Authority
18.	Ministry of Agriculture
19.	Ministry of Lands and Physical Planning
20.	Professional Bodies (EBK, EIK, LSK, ISK, SIMAK)
21.	NEMA
22.	KWS
23.	KFS
24.	KCAA
25.	NLC
26.	National Museums of Kenya
27.	Community Based Organizations (CBO)
28.	Faith Based Organizations (FBOs)
29.	Non-governmental Organizations (NGOs)
30.	Development Partners/Financiers
31.	Political leaders in project areas.
32.	Media
33.	Parliamentary Committee on Energy.
34.	Senate Committee on Energy.
35.	Large power consumers
36.	General Public
37.	Civil Society
38.	KEPSA
39.	Contractors
40.	Sub-Contractors
41.	Consultants

5. NOTICE TO THE PUBLIC

In accordance with the Public Private Partnerships Act, 2021 and the Circular dated 24th April 2025 on Public Disclosure Requirements for PIPs - https://pppkenya.go.ke/ova_doc/circular-on-public-disclosure-of-privately-initiated-proposals-pips/, this disclosure is made to notify members of the public that KETRACO has received the above Privately Initiated Proposals.

The proposals will undergo the statutory processes prescribed under the PPP Act, including evaluation of the proposal, project development activities, stakeholder engagement and negotiations.

6. DISCLAIMER

This public disclosure does not constitute approval of the PIPs. The proposals shall only proceed in accordance with the provisions of the Public Private Partnerships Act, 2021 and all other applicable laws.

Further, any other private party interested in submitting a similar proposal for any of the above projects is invited to submit a written expression of interest to KETRACO within **twenty-one (21) days** from the date of publication of this notice.

7. CONTACT DETAILS

Contracting Authority: Kenya Electricity Transmission Company (KETRACO)
Accounting Officer: Eng. Kipkemoi Kibias, Acting Managing Director
Physical Address: Kawi House, South C, Popo Road, Off Red Cross Road
Postal Address: P.O. Box 34942 - 00100, Nairobi
Telephone: +254 20-4956000/+254 719 018000/+254 732 128000
Email: pips@ketraco.co.ke

Mageuzi ya madini yalenga kuinua wachimbaji wadogo

NA SADIK HASSAN (KNA)

Idara ya Serikali ya Madini imezindua zoezi la ushirikishwaji wa umma kote nchini kuhusu miswada, sera na kanuni zinazopendekezwa kwa lengo la kuleta mageuzi katika sekta ya madini nchini Kenya kupitia kuvutia uwekezaji, kuimarisha usalama na afya mahali pa kazi pamoja na ulinzi wa mazingira, na kuboresha ustawi wa wachimbaji madini na jamii zinazoishi karibu na maeneo ya uchimbaji. Mageuzi ya kisheria yanayopendekezwa yanajumuisha Rasimu ya Mswada wa Vilipuzi ya mwaka 2026, Sera ya Madini, Uchimbaji na Uongezaji Thamani wa Madini, Kanuni za Ada za Vilipuzi, na Kanuni za Afya, Usalama na Mazingira Migodini. Mageuzi hayo yanalenga kuboresha na kuifanya sekta ya madini iendane na maendeleo ya kisasa, kuimarisha utawala bora, na kuoanisha sekta hiyo na viwango na mbinu bora vinavyoibuka duniani. Akizungumza wakati wa kongamano la ushirikishwaji wa umma lililofanyika Mombasa, Mkurugenzi wa Leseni, Uzingatiji wa Sheria na Utekelezaji katika Wizara ya Madini, Uchumi wa Buluu na Masuala ya Bahari, Gregory Kituku, alisema Kanuni za Afya, Usalama na Mazingira Migodini za mwaka 2026 zitachukua nafasi ya kanuni za zamani zilizotungwa chini ya Sheria ya Madini (Sura ya 306) ambayo ilifutwa. Kituku alisema mfumo huo mpya wa kanuni umeandaliwa ili kukidhi mahitaji yanayobadilika ya sekta ya madini, hususan kutokana na ukuaji wa haraka wa uchimbaji mdogo



1. **Wakazi wafuatilia matukio wakati wa kongamano la ushiriki wa umma kuhusu marekebisho yaliyopendekezwa ya sheria na kanuni za madini katika Kaunti ya Mombasa.**
2. **Afisa wa Wizara ya Madini Gregory Kituku akitoa taarifa kwa KNA pembezoni mwa kongamano la ushiriki wa umma kuhusu sheria na kanuni zilizopendekezwa za madini katika Kaunti ya Mombasa.**

wa madini na uchimbaji wa kienyeji (ASM), huku ukihamasisha shughuli salama zaidi za uchimbaji na mbinu endelevu za kuhifadhi mazingira. Kwa mujibu wa Idara ya Serikali ya Madini, sekta ya uchimbaji mdogo na wa kienyeji kwa sasa inaajiri takribani watu 14,000 moja kwa moja na kusaidia zaidi ya Wakenya

800,000 kujipatia riziki kupitia shughuli za kiuchumi zinazohusiana na uchimbaji madini. Licha ya mchango wake katika kuboresha maisha ya wananchi, sekta hiyo ambayo kwa kiasi kikubwa hufanyika isivyo rasmi inaendelea kukabiliwa na changamoto kubwa za afya, usalama na mazingira. Ajali za mara kwa

maru zimekuwa zikiwaweka wachimbaji katika hatari za kikazi zinazochangia majeraha na vifo. Kituku alisema kanuni zinazopendekezwa zinalenga kulinda afya, usalama na ustawi wa watu wote wanaofanya kazi migodini pamoja na wale wanaotembelea maeneo ya uchimbaji. Pia zinaweka hatua za kuhakikisha shughuli za utafutaji, uchunguzi na uchimbaji wa madini zinafanywa kwa usalama, uwajibikaji na kwa kuzingatia viwango vinavyokubalika vya utunzaji wa mazingira. Alibainisha kuwa kanuni hizo pia zinaweka kulinda jamii zinazozunguka migodi dhidi ya athari za kiafya na kimazingira zinazotokana na shughuli za uchimbaji, huku zikiimarisha ufuatiliaji wa usalama kazini, usimamizi wa mazingira na uzin-

gatiaji wa sheria katika sekta hiyo. "Kanuni hizi tunazoandaa zinalinga kuimarisha usalama wa wafanyakazi na waendeshaji wa migodi mikubwa, migodi midogo na wachimbaji wa kienyeji," alisema Kituku. Alieleza imani kuwa mfumo huo mpya wa kisheria utapunguza kwa kiwango kikubwa ajali na kuboresha uzingatiji wa sheria mara utakapoanza kutekelezwa. Mkurugenzi huyo alisema kanuni hizo zinaanzisha sura mpya kuhusu urejeshaji wa migodi katika hali yake ya awali, ikiwemo kuanzishwa kwa leseni ya urejeshaji wa migodi ambayo haikuwepo hapo awali. Sharti hilo jipya litahakikisha maeneo ya uchimbaji yanarejeshwa katika hali salama baada ya shughuli za utafutaji na uchimbaji kukamilika, hivyo kupunguza uharibifu wa mazingira wa muda mrefu.

Kituku alisema Rasimu ya Mswada wa Vilipuzi ya mwaka 2026 inalenga kufuta Sheria ya sasa ya Vilipuzi (Sura ya 115), ambayo imekuwa ikitumika kwa zaidi ya miaka 100 na ambayo haikidhi tena maendeleo ya sasa ya teknolojia na uendeshaji katika usimamizi wa vilipuzi vya kibiashara. Sheria inayopendekezwa inaweka msingi wa kuanzishwa kwa Kurugenzi ya Vilipuzi vya Kibiashara na Ukaguzi, ambayo itasimamia, kudhibiti na kufuatilia utengenezaji, uhifadhi, usafirishaji, uuzaji na matumizi ya vilipuzi vya kibiashara nchini kote. Alisema muswada huo pia unaanzisha mbinu za kisasa za kuchunguza malalamiko yanayohusiana na shughuli za ulipuaji, ikiwemo madai ya uharibifu wa mali unaosababishwa na vilipuzi, pamoja na kuweka taratibu zilizo wazi zaidi za kutathmini na kutatua migogoro hiyo. Sheria hiyo inayopendekezwa pia inaleta marekebisho ya ada za leseni za vilipuzi, huku Kituku akieleza kuwa ada zilizopo kwa sasa zimepitwa na wakati na haziakisi gharama halisi za udhibiti na utoaji wa huduma.

Mfumo mpya kuboresha ukaguzi na matengenezo ya madaraja nchini

NA JOSEPH NG'ANG'A (KNA)

Wizara ya Barabara na Uchukuzi imezindua Miongozo ya Mfumo wa Usimamizi wa Madaraja (Bridge Management System - BMS), hatua muhimu inayolenga kuimarisha ukaguzi, matengenezo na usimamizi wa miundombinu ya madaraja nchini Kenya. Waziri wa Barabara na Uchukuzi, Davis Chirchir, alisema mfumo huo mpya utaimarisha usalama wa madaraja, kuboresha mipango ya matengenezo na kuongeza muda wa matumizi ya miundombinu muhimu ya usafiri. Alisema mtandao wa barabara nchini Kenya una urefu

wa zaidi ya kilomita 240,000 zinazojumuisha barabara za kitaifa na za kaunti, huku zaidi ya makaravati ya sanduku (box culverts) 5,100 yakisaidia kuunganisha maeneo mbalimbali kupitia njia kuu za usafiri. "Hata hivyo, miundombinu inayochakaa, ukosefu wa ukaguzi wa kutosha, rekodi zilizotawanyika, rasilimali finyu za matengenezo na kuongezeka kwa athari za mabadiliko ya tabianchi kumeweka madaraja katika hatari ya kuharibika na kudhoofika kwa miundo yake," alisema Waziri. Katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Katibu Mkuu wa Idara ya Barabara, Mhandisi Joseph Mbugua, jijini Nairobi, Chirchir alisema uzinduzi huo ni



Katibu wa Wizara ya Barabara, Mhandisi Joseph Mbugua, akizungumza jijini Nairobi wakati wa uzinduzi wa miongozo ya Mfumo wa Kusimamia Madaraja (BMS).

hatua kubwa katika kuboresha usimamizi wa mali za madaraja nchini kupitia matumizi ya mfumo wa viwango vya pamoja unaotegemea takwimu na unaosisitiza matengenezo ya kinga. "Miongozo hiyo minane inatoa maelekezo ya kina kwa taasisi za usimamizi wa barabara kuhusu namna ya kulinda miundombinu muhimu, kuimarisha usalama wa

wananchi, kuboresha matumizi ya rasilimali, kuhakikisha thamani ya fedha za umma na kuongeza uwezo wa miundombinu kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi," alisema Chirchir. Alibainisha kuwa Kenya ina zaidi ya madaraja 3,100 yanayoweza usafiri, biashara na ukuaji wa uchumi. Miongozo hiyo imeandaliwa kwa

ushirikiano na msaada wa Shirika la Ushirikiano wa Kimataifa la Japan (JICA), na inaweka taratibu za pamoja za ukaguzi wa madaraja, tathmini ya hali yake, upangaji wa matengenezo na utekelezaji wa ukarabati, hatua zitakazoweza taasisi za usimamizi wa barabara kupanga vipaumbele vya uwekezaji na kuimarisha uimara wa madaraja. Kwa upande wake, Katibu huyo aliishukuru Serikali ya Japan pamoja na JICA kwa kuendelea kutoa msaada wa kiufundi, akisema ushirikiano huo umeimarisha uwezo wa taasisi na kuendeleza usimamizi endelevu wa mali za madaraja nchini Kenya. Mfumo wa usimamizi wa madaraja utawezesha ukusanyaji wa taarifa za ukaguzi kwa utaratibu, utoaji wa viwango vya pamoja vya kutathmini hali ya madaraja, pamoja na kupanga kwa uwazi vipaumbele vya matengenezo. Hii itasaidia taasisi za barabara kutumia rasilimali kwa ufanisi, kuboresha usalama na kuhakikisha thamani bora ya uwekezaji wa fedha za umma.

Ukarabati wa Bwawa la Kenyatta kupanua unyunyiziaji Msitu wa Mau

NA PENINA KIIHIKA (PCO)

Idara ya Serikali ya Umwagiliaji itakarabati Bwawa la Kenyatta lililoko ndani ya Msitu wa Mau ili kuimarisha shughuli za umwagiliaji na kuboresha maisha ya wananchi kupitia Mpango Jumuishi wa Uhifadhi wa Msitu wa Mau na Uboreshaji wa Maisha (MFC-ICLIP). Mradi huo wa ukarabati unatarajiwa kunufaisha takriban kaya 1,800 kwa kusaidia umwagiliaji wa wakulima wadogo katika eneo la takriban ekari 1,200, hatua itakayoozeka uzalishaji wa chakula huku ikiimarisha juhudi za uhifadhi wa mnara mkubwa zaidi wa maji nchini. Hatua za Idara ya Serikali zitahusisha ujenzi wa kituo cha kusukuma maji kinachotumia nishati ya jua, ukarabati wa kingo za bwawa, ujenzi wa tanki la kuhifadhi maji lenye uwezo wa mita za ujazo 300, uwekaji wa mfumo wa usambazaji wa maji utakao hudumia ekari 1,200, pamoja na utoaji wa vifaa vya umwagiliaji wa matone kwa bustani za shule. Mradi huo unakadiriwa kugharimu Shilingi milioni 480. Mkurugenzi wa Urejeshaji wa Ardhi na Ustahimilivu wa Tabianchi kwa Usalama wa Maji na Chakula, Thandi Githae, katika Jimbo la Kuresoi Kaskazini, Kaunti ya Nakuru. Wakati wa ziara hiyo, Mama wa Taifa alipitisha rasmi eneo la hekta 33 la Msitu wa Bararget katika sehemu ya Marindas, ambapo ataongoza shughuli za upandaji miti na utunzaji wa msitu chini ya Mpango Jumuishi wa Uhifadhi wa Msitu wa



Mke wa Rais Rachel Ruto (kulia) akikaribishwa na Mkurugenzi wa Urejeshaji Ardhi na Ustahimilivu wa Tabianchi kwa Usalama wa Maji na Chakula, Thandi Githae, katika Jimbo la Kuresoi Kaskazini. PICHA: BENEDICT WASICHE/KNA

Mau na Uboreshaji wa Maisha. Pia alizindua Mradi wa Mashamba ya Matunda katika Shule ya Msingi ya Baringo. Katibu Mkuu wa Wizara ya Mazingira, Mhandisi Festus Ng'eno, alisema mradi huo utatumika kama kituo cha mfano cha mafunzo ambapo wakulima watapata ujuzi wa vitendo kuhusu urejeshaji wa mazingira na njia endelevu za kujipatia riziki. Kupitishwa kwa eneo hilo la hekta 33 ni sehemu ya mkakati mpana wa serikali wa kurejesha Msitu wa Mau. Mpango huo wa urejeshaji ulianzishwa mwezi Julai 2025 na kuzinduliwa rasmi Oktoba mwaka

huo huo, huku Mhandisi Ng'eno akiwa mlezi wa mpango wa uhifadhi na uboreshaji wa maisha. Akizungumza na wakazi, Mama wa Taifa aliwahimiza Wakenya kupanda miti zaidi ili kuongeza eneo la misitu na kuimarisha usalama wa chakula. Aliwapongeza wanajamii kwa kulima viazi mwingi katika maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya urejeshaji wa msitu, akisema hatua hiyo inaboresha maisha yao huku ikiunga mkono juhudi za uhifadhi. Alisisitiza kuwa jamii zinazoiishi karibu na Msitu wa Mau

KWA TAKWIMU

1,800

Mradi unatarajiwa kunufaisha takriban familia 1,800 kwa kusaidia umwagiliaji mdogo katika ekari 1,200 za ardhi, kuongeza uzalishaji wa chakula huku ikiimarisha juhudi za uhifadhi katika mnara mkubwa zaidi wa maji nchini.

zinapaswa kuwa kitovu cha shughuli za urejeshaji kwa kuwa mfumo huo wa ikolojia ni chanzo muhimu cha maji kinachotegemewa na maelfu ya wananchi nchini kwa maisha yao. Mama wa Taifa alisema ushiriki endelevu wa jamii utahakikisha mafanikio ya muda mrefu ya juhudi za urejeshaji huku ukilinda rasilimali za maji, bioanuwai na uzalishaji wa kilimo kwa vizazi vijavyo. Kwa upande wake, Mhandisi Ng'eno alisema Mpango Jumuishi wa Uhifadhi wa Msitu wa Mau na Uboreshaji wa Maisha unashirikiana na mpango wa "Mama Doing Good" kuanzisha bustani za shule zinazolenga kuboresha lishe ya wanafunzi huku ziki-kuza uhifadhi wa mazingira. Alisema mpango huo unatambua watoto wa shule kuwa mabalozi muhimu wa mazingira wanaoweza kuhamasisha maadili ya uhifadhi katika familia na jamii zao. Chini ya mpango huo, mashamba ya matunda yataanzishwa awali katika shule 108 zilizoko ndani ya Msitu wa Mau, huku kila shule ikipokea miche 40 ya parachichi. Baadaye, mpango huo utapanuliwa hadi kufikia shule zote 534 zilizopo ndani ya mfumo wa ikolojia wa msitu huo. Serikali inatarajia kuwa mashamba ya matunda na bustani za shule zitaboresha lishe, kutoa fursa za kujifunza kilimo kwa vitendo na kuimarisha utunzaji wa mazingira miongoni mwa wanafunzi. Miongoni mwa waliohudhuria hafla hiyo walikuwa Balozi Idah Odinga, Makatibu wa Mawaziri kutoka Wizara za Mazingira, Mabadiliko ya Tabianchi na Misitu pamoja na Wizara ya Jinsia, Utamaduni, Sanaa na Urithi, miongoni mwa wengine.

Chama cha Ushirika wa Maziwa Kericho chapigwa jeki ya Sh10m

NA KELOX MUTAI (KNA)

Sekta ya ufugaji wa ng'ombe swa maziwa katika Kaunti ya Kericho inatarajiwa kupata msukumo mkubwa baada ya Chama cha Ushirika cha Wakulima wa Maziwa cha Cherobu kilichopo Wadi ya Cheboin, Kaunti Ndogo ya Bureti, kupokea ruzuku ya Shilingi milioni 10 kupitia Mpango wa Maendeleo ya Biashara (Enterprise Development Programme - EDP) chini ya Mradi wa Kitaifa wa Maendeleo ya Mnyororo wa Thamani ya Kilimo (National Agricultural Value Chain Development Project - NAVCDP). Fedha hizo zitatumika kuimarisha uchakataji wa maziwa, kupanua shughuli za kuongeza thamani ya mazao na kuboresha mapato ya mamia ya wakulima wadogo wa maziwa. Kwa mujibu wa Gavana wa Kericho, Dkt. Erick Mutai, chama hicho kwa sasa hukusanya zaidi ya lita 15,000 za maziwa kila siku

kutoka kwa wakulima wa maeneo jirani na kina uwezo wa kuongeza kiwango hicho hadi zaidi ya lita 25,000 mara tu miundombinu yake ya uchakataji itakapoboreshwa kikamilifu. Alisema hatua hiyo itakiweka chama hicho katika nafasi muhimu ya kuongoza mageuzi ya sekta ya maziwa katika kaunti hiyo. Alieleza kuwa ruzuku hiyo itakiwezesha chama kupanua shughuli za kuongeza thamani ya maziwa, kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvunwa na kuboresha upatikanaji wa masoko yenye thamani kubwa, hatua ambayo itaongeza faida kwa wakulima katika mnyororo mzima wa thamani wa sekta ya maziwa. Akizungumza na wakazi na wadau wakati wa utoaji wa ruzuku hiyo katika Wadi ya Cheboin, Dkt. Mutai alisema serikali ya kaunti imeamua kubadili mwelekeo kutoka kuuza maziwa ghafi kwenda kuongeza thamani kupitia uwekezaji katika



Gavana wa Kaunti ya Kericho, Dkt. Erick Mutai, akihutubia wakazi wakati wa kukabidhi ruzuku ya Shilingi milioni 10 ya EDP kwa Chama cha Ushirika wa Maziwa cha Wakulima cha Cherobu katika Wadi ya Cheboin, Kaunti Ndogo ya Bureti. PICHA: KELOX MUTAI

miundombinu ya uchakataji na kuimarisha vyama vya ushirika. "Uwekezaji huu unalenga kuimarisha shughuli za kuongeza thamani ili wakulima wasiwe wazalishaji wa maziwa ghafi pekee, bali washiriki kikamilifu katika uchakataji wa maziwa. Hii

itawawezesha kupata mapato ya kudumu na ya juu zaidi kutokana na bidhaa za maziwa zilizoongezwa thamani ambazo hupata bei nzuri sokoni," alisema Dkt. Mutai. Alisisitiza kuwa mpango huo unatarajiwa kuboresha ufanisi wa ushughulikiaji wa maziwa,

kupunguza upotevu wa mazao baada ya kuvunwa na kuanzisha vyanzo endelevu vya mapato kwa familia zinazojihusisha na ufugaji. Aidha, alisema vyama vya ushirika vinaendelea kuwa nguzo muhimu ya mabadiliko ya uchumi wa maeneo ya vijijini na kuwawezesha wakulima. Gavana huyo pia alibainisha kuwa serikali ya kaunti imeendelea kupitia vyama vya ushirika vya maziwa miundombinu muhimu ikiwemo mitambo ya kupooza maziwa, mashine za kuchanganya malisho, matreka na vifaa vingine vinavyolenga kuongeza uzalishaji na kudemisha viwango vya ubora. "Tunajenga mnyororo kamili wa thamani wa sekta ya maziwa ambapo maziwa hayazalishwi tu, bali pia yanashughulikiwa ipasavyo, yanapozwa, yanachakatwa na kuuzwa kwa njia inayoongeza faida kwa wakulima huku ikipunguza hasara katika kila hatua ya mnyororo wa thamani," alieleza Dkt. Mutai.

MAKALA: UWEZESHAJI WA AKINA MAMA

Namna kilimo kilivyobadilisha maisha ya waliokuwa watengenezaji wa chang'aa katika Elgeyo Marakwet

NA ALICE WANJIRU NA JUNE JEBET (KNA)

Wakiwa wamevalia sare zao rasmi za blauzi nyeupe na sketi nyeusi, wanachama wa kikundi cha Women for Change wanaonyesha nidhamu na mpangilio wanapoendelea na shughuli yao mpya ya kujipatia riziki. Ukiwaona wakilima mashamba yao kwa bidii na ari kubwa, ni vigumu kuamini kuwa waliwahi kupitia maisha ya taabu yaliyokatizwa mara kwa mara na misako ya polisi katika maeneo ya kutengeneza pombe haramu—maeneo yaliyogubikwa na vurugu, ambako walevi walikuwa wakiyumbayumba kutokana na ulevi.

Leo hii, wanawake hawa wamepata mwelekeo mpya na matumaini mapya maishani. Hata hivyo, kwa miaka mingi walitegemea utengenezaji wa pombe haramu, ikiwemo chang'aa, kama njia yao pekee ya kujikimu.

Kwa miongo kadhaa, waliendelea kuamini kuwa kutengeneza chang'aa ndiko kulikuwa chanzo chao pekee cha mapato. Kwa mshangao wao, baadaye waligundua kuwa walikuwa wamekua juu ya hazina kubwa muda wote—ardhi yenye rutuba ambayo ingeweza kulisha familia zao na kuwapatia kipato endelevu kupitia kilimo. Kilichokosekana ni maarifa, mwongozo na mtazamo sahihi wa kuitumia ipasavyo.



Wajumbe wa Wanawake wa Mabadiliko ambao walikuwa watengenezaji wa pombe wa zamani wakati wa sherehe za Siku ya Kimataifa ya Kupinga Matumizi Mabaya ya Dawa za Kulevya na Usafirishaji Haramu katika eneo la Metkei katika Kaunti Ndogo ya Keiyo Kusini.

Hadithi ya Ruth Chepkok inaakisi maisha ya wanawake wengi katika kikundi hicho, ambacho wanachama wake wameenea katika Kaunti ya Elgeyo Marakwet. Muda mfupi baada ya kuolewa, Bi. Chepkok alitambulishwa katika biashara ya kutengeneza pombe haramu katika familia ya mumewe, ambapo ilikuwa chanzo pekee cha mapato ya familia. Kwa miaka 15, alitumia siku zake akichemsha mapipa ya pombe yenye sumu. Licha ya hatari ya kukamatwa kila mara na ugumu wa kazi hiyo, haku-

pata chochote cha kujivunia. Biashara hiyo haikumfanya kuwa maskini kifedha pekee, bali pia iliisambaratisha familia yake. Yeye pamoja na mumewe hawakuwa tu wakiuza pombe haramu bali pia waliitumia. Mwaka 2011, mume wake alifariki kutokana na matatizo ya kiafya yaliyotokana na matumizi ya pombe. “Baada ya kifo chake, maisha yangu yalivurugika kabisa,” anakumbuka. “Kutambua kwamba nilipaswa kukabiliana na maisha pekee yangu bila mtu wa kunitegemea kulinisukuma zaidi katika msongo wa mawazo. Nilianza kunywa pombe kupita kiasi, na maisha yangu yakazidi kuzorota.” Katika miaka hiyo ya giza ya uraibu wa pombe, Bi. Chepkok alipuuza hata usafi wake binafsi na mara chache sana alioga. Akiwa na hamu kubwa

ya kuendeleza uraibu wake, alianza kuuza mali za nyumbani moja baada ya nyingine. Hatimaye, aliuza karibu kila kitu alichokuwa nacho, ikiwemo magodoro ya familia, na hivyo kulazimika yeye pamoja na watoto wake kulala sakafuni kwenye baridi kali. Mabadiliko yake yalianza mwaka 2015 kufuatia mabadiliko ya kimkakati yaliyofanywa na Serikali ya Kaunti ya Elgeyo Marakwet kwa kushirikiana na NACADA. Baada ya kutambua kuwa utekelezaji wa sheria kwa njia ya adhabu pekee haukuwa ukileta matokeo ya kudumu, viongozi wa kaunti waliamua kuwashirikisha watengenezaji wa pombe haramu moja kwa moja ili kuwabadilisha kutoka ndani na kupata matokeo ya kudumu. Hatua hiyo ilisababisha ushirikiano rasmi na shirika la Empowering Lives

International (ELI), ambao ulimpa Bi. Chepkok fursa mpya ya kubadili maisha yake.

Leo, maisha yake yamebadilika kabisa kiroho, na kwa sasa anasomea kuwa mchungaji. Ingawa bado hajawekwa wakfu rasmi, tayari anatomia ushuhuda wa maisha yake kuwaokoa wanawake wengine kutoka katika minyororo ya uraibu wa pombe na utengenezaji wa pombe haramu.

Bi. Peris Kiprof pia ana simulizi yenye maumivu makubwa. Kwa miaka 10 aliyotumia akitengeneza pombe haramu, maisha yake yalidhoofika sana kutokana na athari za kazi hiyo na matumizi makubwa ya pombe kiasi kwamba wakazi wa eneo hilo walimpa jina la dhahaka la “mtisho wa ndege” kwa sababu ya mwonekano wake.

Kama ilivyokuwa kwa Bi. Chepkok, Bi. Kiprof alipata ukombozi kupitia programu hiyo na akaamua kuishi maisha ya kumtumikia Mungu. Tayari amewekwa wakfu rasmi kuwa mchungaji na anahudumu kama mchungaji mshauri wa kikundi hicho.

Kwa pamoja, Bi. Chepkok na Bi. Kiprof wamekuwa nguzo za msaada wa kihisia na kiroho kwa wana-chama wa kikundi hicho. Wanatumia uzoefu wao binafsi kuwapa ushauri wa kweli na matumaini wale ambao bado wamenaswa katika biashara ya kutengeneza pombe haramu.

Nyamira kugatua huduma za figo hadi kwa hospitali za ngazi ya kaunti ndogo

NA DEBORAH BOCHERE (KNA)

Gavana wa Kaunti ya Nyamira, Amos Nyaribo, amewahakikishia wakazi kuwa serikali ya kaunti imejipanga kuanzisha vitengo vya huduma za figo katika hospitali za ngazi ya kaunti ndogo ili kuwapatia wananchi huduma za usafishaji damu (dialysis) karibu na makazi yao na kupunguza msongamano katika Hospitali ya Rufaa ya Kaunti ya Nyamira. Akizungumza katika Hospitali ya Rufaa ya Nyamira wakati wa uzinduzi wa kitengo kipya cha huduma za dialysis katika Doctor's Plaza, Gavana Nyaribo aliwahimiza wagonjwa wenye matatizo ya figo kutumia mashine na huduma zilizowekwa.

“Ninazindua mashine 10 za dialysis kwa Hospitali ya Rufaa ya Nyamira. Mipango ya kununua mashine nyingine 30 iko katika hatua za mwisho. Kati ya mashine hizo 30, mashine 10 zitapelekwa Hospitali ya Kaunti Ndogo ya Keroka, mashine 10 Hospitali ya Kaunti Ndogo ya Ekereny, na mashine 10 zilizobaki zitawekwa hapa Hospitali ya Rufaa ya Nyamira. Kabla ya uzinduzi wa leo, Nyamira ilikuwa na mashine tatu pekee; hivyo baada ya kupokea mashine zote, hospitali hii itakuwa na jumla ya mashine 23, huku ikihudumia wagonjwa wengi, wakiwemo wanaotoka kaunti jirani,” alisema gavana huyo. “Ninawasihi wagonjwa wenye matatizo ya figo na magonjwa



Gavana wa Nyamira, Amos Nyaribo, anazindua kitengo kipya cha figo katika Hospitali ya Rufaa ya Nyamira na kuzungumza na wagonjwa wanaosubiri kufanyiwa matibabu ya kusafisha damu (dialysis).

PICHA: DEBORAH BOCHERE

mengine yanayohusiana kutafuta matibabu mapema na kudhibiti hali hii ambayo kwa sasa inaathiri watu wa rika zote,” aliongeza. Mashine mpya zilizozinduliwa katika Hospitali ya Rufaa ya Nyamira zitawaweza sha wahudumu wa afya kutoa huduma za dialysis kwa wagonjwa 26 kila siku.

Kitengo cha huduma za figo katika Hospitali ya Rufaa ya Nyamira kimehamishwa kutoka wodi za kawaida hadi katika eneo jipya lenye nafasi kubwa, kituo cha wauguzi na huduma nyingine muhimu. “Serikali yangu itanunua kemikali na vifaa zaidi vya dialysis pamoja na kuajiri wahudumu

wa afya zaidi ili kukidhi mahitaji ya wagonjwa na kudumisha ubora na ufanisi wa huduma. Msikate tamaa mnapokuja kupata huduma za dialysis. Utaratibu huu unaweza kuongeza muda wa maisha yenu huku mkitafuta fursa ya kupandikizwa figo,” Gavana Nyaribo aliwahimiza wagonjwa. Mgonjwa mmoja, Bw. Joseph Omwando, alisema sasa hat-alazimika tena kutumia saa nyingi akisubiri zamu yake ya kupata huduma za dialysis. “Tulikuwa tukilazimika kufika hospitalini ifikapo saa kumi alfajiri ili tusajiliwe mapema na kupata nafasi kwenye foleni kutokana na uchache wa mashine. Ninamshukuru gavana kwa kuongeza mashine na kwa mpango wake wa kupeleka huduma hizi katika hospitali za kaunti ndogo ili tusilazimike kusafiri hadi Nyamira kupata huduma hizi muhimu kwa maisha yetu,” alisema Omwando. Mgonjwa mwingine, Bw. Julius Bosire, alieleza mateso aliyopitia alipokuwa akitafuta huduma za dialysis nje ya kaunti.



DISCLOSURE ON THE PROJECT AGREEMENT FOR GILGIL – NAKURU – MAU SUMMIT (A8) PPP ROAD PROJECT

A: BACKGROUND:

The Kenya National Highways Authority (KeNHA) received a Privately Initiated Proposal (PIP) from Shandong Hi-Speed Road & Bridge International Engineering Co. Ltd (SDRBI) for the Design, Build, Finance, Operate, Maintain and Transfer (DBFOMT) of the Gilgil - Nakuru - Mau Summit (A8) Road i.e. approximately 94 Km of the A8 Highway between Gilgil and Mau Summit. The Project road traverses two counties namely Nakuru and Baringo. The PIP was granted conditional approval to proceed to Project Development Phase (PDP) by the PPP Committee after which the Project Proponent undertook Project Development Phase (PDP) activities/ Feasibility Studies and submitted a Feasibility Study Report.

Pursuant to the submissions, the Contracting Authority evaluated the Project Development Phase documentation in accordance with the provisions of Section 43(9) of the PPP Act, Cap 430. The Evaluation Report, prepared in compliance with Section 43, identified Shandong Hi-Speed Road & Bridge International Engineering Co. Ltd (SDRBI) as the Preferred Proponent to undertake the project road section, as per Section 55(1)(d) of the PPP Act. The PPP Committee subsequently delivered its decision during its 48th Extraordinary PPP Committee meeting held on 10th November, 2025 to the effect that the Committee adopted the recommendations of the Evaluation Report, which identified SRDBI as the Preferred Proponent for the Gilgil - Nakuru - Mau Summit (A8) Road, subject to the fulfilment of the conditions outlined in the Evaluation Report.

The Contracting Authority commenced negotiations with the Proponent and subsequently submitted the Project and Financial Risk Assessment Report together with the initialed Project Agreement to the PPP Directorate for its recommendations, and thereafter to the PPP Committee for approval in accordance with Section 58 (1) and 58 (2) of the PPP Act, Cap 430.

B: NOTICE TO THE PUBLIC:

In this regard, the Contracting Authority (KeNHA), the PPP Directorate, and the PPP Committee have undertaken the necessary processes and procedures in line with the provisions of the PPP Act, Cap 430 in processing the Privately Initiated Proposal and hereby notify the public of the following:

The PPP Committee delivered its decision during its 56th Ordinary meeting held on 25th November, 2025 to the effect that the Committee:

1. **Approved** the Project and Financial Risk Assessment Report and the execution of a Project Agreement between the Contracting Authority and the SDRBI pursuant to section 59 (2) of the PPP Act, Cap 430.
2. **Directed** the Contracting Authority to publish a disclosure notice disclosing all information permitted for publication under the PPP Act, the PPP Regulations and applicable confidentiality provisions.

Following the initialed Project Agreement, the Contracting Authority (KeNHA) signed an Early Works Agreement and has subsequently executed the Project Agreement with the Project Proponent (SDRBI) to enable the commencement of the Works.

The Project Agreement, as highlighted in the background above, covers a total of 94 kilometers on the A8 Road. The project will be delivered by Shandong Hi-Speed Road & Bridge International Engineering Co. Ltd (SDRBI) under a Design, Build, Finance, Operate, Maintain, and Transfer (DBFOMT) PPP arrangement for a period of thirty (30) years.

Summary of Key Project Features:

Feature	Project Information
Nature of the Project and Key Terms of the Project Agreement	The Project is being implemented as a Design, Build, Finance, Operate, Maintain and Transfer (DBFOMT) Public Private Partnership (PPP) for the development of the Gilgil - Nakuru - Mau Summit (A8) Road. The Project Agreement provides for the design, financing, construction, operation, maintenance and eventual transfer of the Project assets to Kenya National Highways Authority (KeNHA) at the end of the concession period.
Works to be Developed / Public Services to be Performed	The Project comprises the design, financing, construction, operation and maintenance of approximately 94 kilometers of the A8 Road, including associated interchanges, viaduct in Nakuru City, bridges, drainage structures, tolling infrastructure, road safety features, and other ancillary facilities required to provide a safe and efficient highway service.
Successful Bidder / Project Proponent	Shandong Hi-Speed Road & Bridge International Engineering Co. Ltd (SDRBI)
Amount of Public Funds Committed to the Project	The Government's financial commitments under the Project Agreement are limited to those expressly provided for therein. The Project is primarily financed by the Private Party, with any Government support being subject to the provisions of the Project Agreement and applicable law.
Project Tariff	The Project will operate as a toll road. Applicable toll tariff is KES 8.50, and any future adjustments shall be implemented in accordance with the Project Agreement and applicable Government approvals and regulatory requirements.
Government Support Measures	Government support measures, where applicable, are provided in accordance with the Project Agreement and the PPP Act, Cap 430, and may include contractual undertakings necessary to facilitate implementation of the Project and manage agreed project risks.
Social and Economic Benefits	The Project is expected to improve road safety, reduce travel time and vehicle operating costs, enhance connectivity between Nairobi and the Rift Valley region, facilitate trade and tourism, create employment opportunities during construction and operation, and stimulate regional economic growth and investment.
Duration of the Project	Thirty (30) years, inclusive of the design, construction, operation, and maintenance period, after which the Project assets will be transferred to KeNHA in accordance with the Project Agreement.
Expected Asset Quality at Handback	Upon expiry or termination of the concession, the Project assets shall be transferred to KeNHA in the condition and quality prescribed under the Project Agreement, having regard to the applicable handback requirements, performance standards and remaining asset life.
Project Monitoring and Reporting	The Project will be monitored by KeNHA throughout the concession period in accordance with the Project Agreement. Monitoring will include compliance with design and construction standards, operational performance indicators, maintenance standards, safety obligations, environmental and social requirements, financial reporting obligations and other contractual performance requirements. The Private Party will be required to submit periodic reports as stipulated in the Project Agreement.

This disclosure is made pursuant to Section 69 (1) of the Public Private Partnerships Act (Cap 430) to notify members of the public of the PPP Committee's decision approving the Project and Financial Risk Report, and the subsequent execution of the Project Agreement between the Kenya National Highways Authority (KeNHA) and the Shandong Hi-Speed Road & Bridge International Engineering Co. Ltd (SDRBI).


Further, this disclosure is made in line with The National Treasury Circular dated 24th April, 2025 on Public Disclosure on Privately Initiated Proposals (https://pppkenya.go.ke/ova_doc/circular-on-public-disclosure-of-privately-initiated-proposals-pips/) and in line with Government of Kenya's desire for transparency in all its initiatives.

KeNHA remains committed to strictly adhering to the provisions of the PPP Act, Cap 430 and further assures the public that it will endeavor to abide by the provisions of the PPP Act Cap 430. The Government of Kenya, similarly remains committed to

delivering critical infrastructure to Kenyans.

Any clarifications or feedback may be channeled through the following contact details:

CONTRACTING AUTHORITY CONTACT DETAILS	
Contact Person:	Eng. Luka Kimeli
Designation:	Director General, Kenya National Highways Authority [KeNHA]
KeNHA Tel No:	020-4954000
E-mail:	dg@kenha.co.ke ; Copy to: ppp@kenha.co.ke

  COUNCIL OF LEGAL EDUCATION			
INSTITUTIONAL LICENSING STATUS AS AT 30TH JUNE 2026			
Under the provisions of Sections 2, 8 (1) (b), 18, 19, 20, 21, 22, 23 and 48 of the Legal Education Act Chapter 16B Laws of Kenya, the following are the ONLY licensed Legal Education Providers and Legal Education Programmes in Kenya as indicated under each respective cluster.			
(a) MASTER OF LAWS PROGRAMME			
	NAME OF INSTITUTION FACULTY/SCHOOL	LICENSED PROGRAMME	STATUS
1	Kenyatta University School of Law	Master of Laws (LL.M.)	License valid until 13th January 2031
2	Strathmore Law School	Master of Laws (LL.M.)	License valid until 17th April 2030
3	Catholic University of Eastern Africa Faculty of Law	Master of Laws (LL.M.)	License valid until 21st September 2028
4	Jomo Kenyatta University of Agriculture & Technology School of Law	Master of Laws (LL.M.)	License valid until 20th June, 2028
(b) BACHELOR OF LAWS PROGRAMME			
1	Umma University School of Law	Bachelor of Laws (LL.B.) & Sharia	License valid until 14th April 2031
2	Chuka University Faculty of Law	Bachelor of Laws (LL.B.)	License valid until 14th April 2031
3	Tharaka University School of Law	Bachelor of Laws (LL.B.)	License valid until 19th December 2030
4	Zetech University School of Law	Bachelor of Laws (LL.B.)	License valid until 14th October 2030
5	Tom Mboya University School of Law	Bachelor of Laws (LL.B.)	License valid until 14th October 2030
6	Daystar University School of Law - Athi River Campus	Bachelor of Laws (LL.B.)	License valid until 9th April 2029
7	University of Embu School of Law	Bachelor of Laws (LL.B.)	License valid until 9th April 2029
8	Kisii University School of Law	Bachelor of Laws (LL.B.)	License valid until 9th April 2029
9	Mount Kenya University School of Law - Parklands Campus	Bachelor of Laws (LL.B.)	License valid until 9th April 2029
10	Riara Law School	Bachelor of Laws (LL.B.)	License valid until 21st September 2028
11	Kenyatta University School of Law	Bachelor of Laws (LL.B.)	License valid until 21st September 2028
12	Jomo Kenyatta University of Agriculture & Technology School of Law	Bachelor of Laws (LL.B.)	License valid until 20th June, 2028
13	Catholic University of Eastern Africa (CUEA) Faculty of Law	Bachelor of Laws (LL.B.)	License valid until 29th November, 2027
14	Strathmore Law School	Bachelor of Laws (LL.B.)	License valid until 29th November, 2027
15	Maseno University School of Law	Bachelor of Laws (LL.B.)	License valid until 29th November, 2027
16	South Eastern University of Kenya School of Law	Bachelor of Laws (LL.B.)	License valid until 29th November, 2027
(c) DIPLOMA IN LAW PROGRAMME			
1	Mount Kenya University School of Law - Parklands Campus Faculty of Law	Diploma in Law	License valid until 9th April 2029
2	Kisii University School of Law	Diploma in Law	License valid until 9th April 2029
3	Kenya School of Law	Diploma in Law (Para Legal Studies)	License valid until 9th April 2029
4	Catholic University of Eastern Africa (CUEA) Faculty of Law	Diploma in Law	License valid until 29th November, 2027
(d) PENDING APPLICATIONS FOR LICENSING AS LEGAL EDUCATION PROVIDERS			
	NAME OF INSTITUTION	LICENSED PROGRAMME	STATUS
1.	Egerton University Faculty of Law	Bachelor of Laws (LL.B.) - Renewal	Institution's application under consideration by Council.
2.	Kabarak University School of Law	Bachelor of Laws (LL.B.) - Renewal	Institution's application under consideration by Council.
3.	Africa Nazarene University School of Law	Bachelor of Laws (LL.B.) - Renewal	Institution's application under consideration by Council.
4.	Moi University School of Law	Bachelor of Laws (LL.B.) - Renewal	Institution's application under consideration by Council.
5.	University of Nairobi Faculty of Law - Parklands Campus	Bachelor of Laws (LL.B.) - Renewal	Institution's application under consideration by Council.
6.	Rongo University School of Law	Bachelor of Laws (LL.B.) - New	Institution's application under consideration by Council.
7.	Kenya Methodist University School of Law	Bachelor of Laws (LL.B.) - New	Institution's application under consideration by Council.
8.	Murang'a University of Technology School of Law	Bachelor of Laws (LL.B.) - New	Institution's application under consideration by Council.
9.	Mount Kenya University School of Law	Master of Laws (LL.M.)	Institution's application under consideration by Council.

Prof. Busalile Jack Mwimali
SECRETARY/CHIEF EXECUTIVE OFFICER
COUNCIL OF LEGAL EDUCATION

30th June 2026



THE NATIONAL TREASURY

INVITATION FOR PUBLIC PARTICIPATION ON THE PUBLIC PRIVATE PARTNERSHIPS (AMENDMENT) BILL, 2026, THE DRAFT PUBLIC PRIVATE PARTNERSHIPS (GENERAL) REGULATIONS, 2026, AND THE DRAFT PUBLIC PRIVATE PARTNERSHIPS (PROJECT MANAGEMENT) REGULATIONS, 2026

SUBMISSION OF MEMORANDA

The National Treasury, through the State Department for Public Investments & Assets Management, the Public Private Partnerships Directorate, calls for review and comments from the public on the:

- Public Private Partnerships (Amendment) Bill, 2026;**
- Draft Public Private Partnerships (General) Regulations 2026; and**
- Draft Public Private Partnerships (Project Management) Regulations 2026, hereinafter referred to collectively as "draft PPP Regulations".**

The National Treasury has scheduled a series of Public Participation Consultation Forums across various regions, commencing on Monday, 13th July 2026, to sensitize the public and solicit their views on the draft documents.

Public participation will be carried out as scheduled below:

S/No	CLUSTERED COUNTIES	VENUE	DATE	TIME
Nyanza/Western Region	Kisumu, Siaya, Kakamega, Vihiga	Kisumu Hotel Kisumu	13 th -14 th July 2026	9.00am - 5.00pm
	Bungoma, Transnzoia, Busia	Kibabii University	13 th -14 th July 2026	9.00am - 5.00pm
	Kisii, Migori, Homabay, Nyamira,	Kisii University Kisii	13 th -14 th July 2026	9.00am - 5.00pm
Coast Region	Mombasa, Lamu, Kilifi, Tana River,	Kenya School of Government Mombasa	16 th -17 th July 2026	9.00am - 5.00pm
	Kwale	Diani Pride Inn Diani Kwale	16 th -17 th July 2026	9.00am - 5.00pm
	Taita Taveta	Taita Taveta University	16 th -17 th July 2026	9.00am - 5.00pm
Rift Valley	Uashin Gishu, Nandi, Baringo, Elgeyo Marakwet, Kericho, West Pokot, Turkana	Eldoret Polytechnic Eldoret	20 th -21 st July 2026	9.00am - 5.00pm
	Nakuru, Narok, Bomet, Nanyuki	Kenya Wildlife Services Naivasha	20 th -21 st July 2026	9.00am - 5.00pm
	Kajiado	County Commissioners Office Kajiado	20 th -21 st July 2026	9.00am - 5.00pm
Eastern/Central	Embu, Meru, Tharaka Nithi	Kenya School of Government Embu	23 rd -24 th July 2026	9.00am - 5.00pm
	Laikipia, Nyeri, Kirinyaga, Muranga	Dedan Kimathi University, Nyeri	23 rd -24 th July 2026	9.00am - 5.00pm
	Kitui, Machakos, Makueni,	Agriculture Institute Kitui	23 rd -24 th July 2026	9.00am - 5.00pm
Nairobi/North Eastern Region	Nairobi, Kiambu, Garissa, Mandera, Wajir, Marsabit, Samburu	Kenyatta International Convention Centre Nairobi	28 th -29 th July 2026	9.00am - 5.00pm

Members of the public are requested to submit representations and written memoranda on the Amendment Bill and draft Regulations.

The draft documents can be found on the National Treasury website <https://www.treasury.go.ke/public-notices/> or at the Public Private Partnerships Directorate website <https://www.PPPkenya.go.ke>.

The representations and written memoranda may be submitted by email to info@PPPkenya.go.ke, addressed to the Principal Secretary, Public Investments & Assets Management.

Hand-delivered memoranda and representations should be addressed to the Director General, Public Private Partnerships Directorate and delivered to the PPP Directorate's offices on **the 6th Floor Kenya Reinsurance Plaza on Taifa Road.**

All representations and memoranda should be received within 21 days following the publication of this advert.

Serikali yawekeza katika magereza kuimarisha urekebishaji wa wafungwa

NA BERNARD MUNYAO
(KNA)

Serikali inawekeza katika miundombinu ya kisasa ya magereza na kuimarisha ushirikiano na wadau wasio wa serikali ili kubadilisha taasisi za marekebisho kuwa vituo vya urekebishaji wa wafungwa, Katibu wa Idara ya Huduma za Marekebisho, Dkt. Salome Beacco, amesema. Akizungumza wakati wa uzinduzi wa jengo jipya la utawala, ofisi tano pamoja na jengo la malazi lililokarabatiwa katika Gereza la Wanawake la GK Murang'a, Dkt. Beacco alisema kuwa mageuzi yanayoendelea yanalinga kuunda taasisi za marekebisho zinazokuza urekebishaji wa wafungwa, kuheshimu utu wa binadamu na kuwawezesha wafungwa kurejea na kujiunga tena kwa mafanikio katika jamii. Dkt. Beacco alisema serikali inaondoka katika mfumo unaojikita zaidi kwenye adhabu na kuelekea mfumo unaozingatia urekebishaji wa wafungwa na haki ya urejesho, akibainisha kuwa miundombinu bora ina mchango mkubwa katika kufanikisha lengo hilo. "Serikali inaendelea kujitolea kuboresha taasisi za marekebisho ili ziweze kuunga mkono ipasavyo urekebishaji wa wafungwa huku zikitoa mazingira salama, yenye utu na ubinadamu kwa wafungwa na maafisa wamagereza," alisema. Katibu huyo alisema idara hiyo inazidi kutumia ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi ili kuharakisha mageuzi, huku akitambua mchango wa washirika wa maendeleo na mashirika ya kiraia katika kuboresha miundombinu ya magereza na ustawi wa wafungwa. Miongoni mwa miradi iliyozin-



Katibu wa Huduma za Marekebisho, Dkt. Salome Beacco akitembelea Gereza la GK Murang'a lililokarabatiwa.



duliwa ni jengo la malazi lililokarabatiwa ambalo limeundwa kutoa mazingira rafiki zaidi kwa watoto wanaoandamana na mama zao waliofungwa gerezani. Jengo hilo lililoboreshwa lina vyumba vikubwa na vyenye vifaa muhimu, vinavyowawezesha akina mama kuwalea watoto wao katika mazingira salama zaidi

na yenye kuheshimu utu wao huku wakutumikia vifungo vyao. Dkt. Beacco alisema uwekezaji wa aina hiyo unatambua mahitaji ya kipekee ya wafungwa wanawake na watoto wao, akiongeza kuwa taasisi za marekebisho zinapaswa kulinda haki na ustawi wa watu wote walioko chini ya uangalizi wa serikali.

Katika hafla hiyo, Mkurugenzi wa shirika la Freedom Within Kenya, Dkt. Mary Waceke, alisema shirika hilo lilishirikiana na Idara ya Huduma za Marekebisho kusaaidia urekebishaji wa akina mama waliofungwa na kuboresha ustawi wa watoto wanaoishi ndani ya taasisi za marekebisho. Alisema kuwa kuweka mazingira bora ya kuishi kwa akina mama na watoto wao kunaboresha ustawi wa kihisia, huimarisha uhusiano wa kifamilia na

huchangia urekebishaji wenye mafanikio pamoja na kuwawezesha kurejea katika jamii. Kwa upande wake, Kiongozi wa Mradi wa Echo Network Africa, Sarah Muhoya, alisisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya serikali na wadau wasio wa serikali katika kuendeleza mageuzi ya sekta ya marekebisho. Alibainisha kuwa kuwawezesha wanawake, wakiwemo walioko katika taasisi za marekebisho, kunaleta manufaa makubwa yanayovuka mipaka ya magereza. "Wanawake wanapowezeshwa, athari zake huonekana katika familia na jamii kwa ujumla, na hivyo kujenga jamii jumuisi, imara na inayoheshimu utu wa binadamu," aliongeza. Akipongeza maboresho yaliyofanywa katika Gereza la Wanawake la GK Murang'a, Katibu Mkuu huyo aliwataka maafisa wa magereza kuzingatia viwango vya juu vya taaluma, uadilifu na nidhamu. Aliwakumbusha kuwa mafanikio ya mageuzi ya sekta ya marekebisho hayategemei tu miundombinu bora bali pia kujitolea na uwajibikaji wa watumishi wanaosimamia taasisi hizo. "Kila afisa amepewa jukumu zito kwa mujibu wa Katiba, sheria za Kenya na imani ya umma. Kuweka wafungwa salama chini ya ulinzi wenu ndilo jukumu lenu kuu. Kila mtu aliyekabidhiwa katika uangalizi wetu lazima abaki salama, alindwe na ahesabiwe katika kipindi chote cha kifungo chake," aliongeza Katibu Mkuu huyo. Hafla hiyo ilihudhuriwa na Kaimu Katibu wa Huduma ya Uangalizi na Ufuatiliaji wa Wafungwa Baada ya Kuachiliwa (Probation and Aftercare Service), Shadrack Kavutai, Mkurugenzi wa Mageuzi katika Huduma ya Magereza ya Kenya, SACGP Ali Athman, pamoja na viongozi wengine.

Kuweka watu katika uangalizi salama kunabaki kuwa jukumu lako kuu. Kila mtu aliyekabidhiwa kwetu lazima abaki salama

Kisima cha maji cha Arera chapunguza uhaba wa maji Garissa

NA ERICK KYALO (KNA)

Mamlaka ya Kitaifa ya Kusi-mamia Ukame (NDMA), kwa ushirikiano na Serikali ya Kaunti ya Garissa, imezindua rasmi kisima cha maji cha Arera kilichokarabatiwa katika Kaunti Ndogo ya Shanta Abaq, hatua ambayo imeboresha kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa maji salama, ya uhakika na endelevu kwa jamii za eneo hilo pamoja na mifugo yao. Mradi huo ulitekelezwa kufuatia kuongezeka kwa shinikizo katika chanzo cha maji cha Arera, hali iliyowaacha wakazi katika hatari ya kukumbwa na uhaba wa maji wa mara kwa mara, vifo vya mifugo na kudorora kwa maisha yao wakati wa vipindi virefu vya ukame. Ukarabati wa kisima hicho uliharimu Shilingi milioni 1.7, na

unatarajiwa kuimarisha maisha ya wafugaji kwa kuhakikisha upatikanaji wa maji ya uhakika kwa matumizi ya nyumbani na mifugo, huku ukipunguza shinikizo kwa vyanzo vingine vya maji ambavyo mara nyingi huzidiwa wakati wa ukame. Akizungumza wakati wa uzinduzi huo, Mkurugenzi Mkuu wa NDMA, Hared Adan, alisema mradi huo ni sehemu ya mkakati wa muda mrefu wa serikali wa kuimarisha uwezo wa jamii kukabiliana na ukame kupitia uwekezaji katika miundombinu imara ya maji ambayo hupunguza athari za ukame na utegemezi wa hatua za dhurura ambazo ni ghali. "Wakati wa ukame uliopita, tulipokea maombi ya mara kwa mara kutoka kwa jamii ya eneo hili ya kutaka kisima hiki kifanyiwe ukarabati baada



Afisa Mkuu Mtendaji wa NDMA, Hared Adan, na Afisa Mkuu wa Maji wa Kaunti ya Garissa, Mohamed Ibrahim, kwa pamoja wanazindua kisima cha Arera kilichokarabatiwa katika Kaunti Ndogo ya Shanta Abaq.

ya mifugo kulazimika kunywa maji kutoka kwenye mashimo yaliyochimbwa kwa mikono, jambo lililosababisha upotevu mkubwa wa maji na matumizi yasiyo na ufanisi ya rasilimali hiyo adimu," alisema Adan. Alieleza kuwa NDMA ilihamasisha rasilimali kwa ajili ya kukarabati

Wakati wa ukame wa hivi karibuni, tulipokea maombi ya mara kwa mara kutoka kwa jamii kufufua kisima

kisima hicho pamoja na kuboresha mfumo wa kuhifadhi maji na wa kunywesha mifugo ili kuhakikisha upatikanaji wa maji kwa njia bora zaidi na endelevu. Mradi huo ulihusisha ujenzi wa mnara wa maji wa chuma uliotengenezwa maalumu, usakinishaji wa matangi mawili ya kuhifadhi maji yenye uwezo wa lita 10,000 kila moja na hivyo kuongeza uwezo wa kuhifadhi maji hadi lita 20,000, ujenzi wa mabwaga manne ya kunywesha mifugo, pamoja na uwekaji wa mabomba na vifaa vinavyohusiana. Mfumo huo mpya umechukua nafasi ya maeneo ya zamani ya kunywesha mifugo yaliyokuwa yakichimbwa kwa mikono, na hivyo kuboresha matumizi ya maji, kupunguza upotevu na kurahisisha mifugo kupata maji safi. Adan alibainisha kuwa uwekezaji katika miundombinu ya maji inayostahimili athari za ukame ni muhimu katika kupunguza madhara ya kibinadamu na kiuchumi yanayosababishwa na ukame katika maeneo kame na nusu kame.

Meli ya kitalii ya Asia yatia nanga Mombasa ikiwa na watalii 717

NA SADIK HASSAN (KNA)

Utalii wa meli za kifahari unchini umefikia hatua muhimu baada ya kuwasili kwa meli ya kifahari MS Viking Yi Dun, meli ya kwanza kabisa ya watalii kusafiri moja kwa moja kutoka Asia hadi Bandari ya Mombasa. Meli hiyo imeleta watalii 717 pamoja na wahudumu 450 katika safari ya kihistoria inayodhihirisha kuongezeka kwa hadhi ya Kenya kama kitovu cha kimataifa cha utalii wa meli za kitalii. Kuwasili kwa meli hiyo kuna-fanya idadi ya meli za kitalii zilizotia nanga katika kituo cha kisasa cha meli za watalii cha Bandari ya Mombasa kufikia tisa katika msimu wa utalii wa meli unaoanzia Oktoba hadi

Juni, zikiwa zimebeba jumla ya watalii 4,889. Hii ni ongezeko la watalii 684 ikilinganishwa na msimu uliopita wa safari hizo. Katika msimu uliopita wa utalii wa meli, jumla ya meli tano zilitia nanga katika Bandari ya Mombasa zikiwa zimebeba watalii 4,205. Kabla ya mwisho wa mwaka 2026, Kenya inatarajiwa kupokea jumla ya meli 20 za kitalii. Meli hiyo ya kifahari yenye bendera ya Norway, ambayo ina umri wa miaka tisa, iliwasili katika Bandari ya Mombasa ikiwa imewabeba watalii wenye shauku kubwa, wengi wao wakitoka Jamhuri ya Watu wa China, pamoja na wageni kutoka mataifa mengine 16. Ikiwa na urefu wa mita 228 na ghorofa 10 juu ya usawa wa maji,



Nahodha wa meli ya MS Viking Yi Dun, Alex Sehlstedt (kushoto), apokea zawadi ya kuadhimisha safari ya kwanza ya meli hiyo nchini kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari ya Kenya, Kapteni William Ruto (kulia).

meli hiyo ilionekana kwa kuvutia ilipoingia taratibu katika kituo cha kisasa cha meli za watalii cha Bandari ya Mombasa. Ina uwezo wa kubeba abiria 930. Watalii hao walipokelewa kwa burudani ya kuvutia kutoka kwa wasanii wa utamaduni wa Wamijikenda, waliowaburudisha kwa nyimbo na ngoma za asili zilizoonyesha utajiri wa urithi

wa Pwani ya Kenya kabla ya kuanza ziara katika baadhi ya vivutio maarufu vya utalii nchini. Nahodha wa meli hiyo, Alex Sehlstedt, alisema safari hiyo ilianza mjini Shanghai nchini China na inapitia bara la Afrika kuelekea Afrika Kusini kabla ya kuhitimishwa mjini Tarragona nchini Uhispania. “Hadi sasa tumekuwa na hali

nzuri ya hewa, na hata leo hali ya hewa ni nzuri kabisa. Siyo ya joto sana kwangu ambaye ni kama dubu wa maeneo ya barafu, hivyo ninaifurahia sana,” alisema Nahodha Sehlstedt. Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Bandari Kenya (KPA), Nahodha William Ruto, alisema kuwasili kwa mara ya kwanza kwa meli ya watalii kutoka Asia ni ushahidi wa kuongezeka kwa mvuto wa Kenya kama kitovu cha kimataifa cha utalii wa meli za kitalii na kuimarika kwa imani ya kampuni za usafiri wa baharini katika Bandari ya Mombasa kama lango muhimu la Afrika Mashariki. “Hili ni jambo ambalo tume-kuwa tukilisubiri kwa muda mrefu. Kama mnavyojua, meli nyingi za watalii zimekuwa zikitoka Ulaya, lakini hii ndiyo ya kwanza kuwasili kutoka Asia,” alisema Nahodha Ruto. Aliwahakikishia wageni kuwa Bandari ya Mombasa ni salama na akasisitiza dhamira ya KPA ya kuhakikisha usalama na faraja ya watalii wote wanaowasili kwa meli za kitalii. ombasa,” alisema

MAKALA: MADINI

Sera mpya ya madini kukomesha usafirishaji wa madini

NA GODFREY WANG'ANYA NA PAUL NYOKECH (KNA)

Wizara ya Madini, Uchumi wa Bluu na Masuala ya Bahari imezindua Rasimu ya Sera ya Madini, Uchimbaji na Uongezaji Thamani wa Madini ya mwaka 2026, mfumo mpana unaolenga kuibadilisha sekta ya madini nchini kutoka mchango wake wa sasa wa takriban asilimia moja ya Pato la Taifa (GDP) hadi asilimia 10 ifikapo mwaka 2030. Sera hiyo inaashiria hatua muhimu katika juhudi za Kenya kufungua uwezo kamili wa rasilimali zake za madini na kuiweka sekta hiyo kuwa kichocheo kikuu cha ukuaji wa viwanda, uundaji wa ajira na kuongeza mapato yatoakanayo na mauzo ya bidhaa nje ya nchi. Akizungumza wakati wa mkutano wa wadau uliofanyika katika Ukumbi wa Magharibi Hall mjini Kakamega, Mkaguzi wa Madini Philip Kirui alisema sera hiyo imejengwa juu ya msingi uliowekwa na Sheria ya Madini ya mwaka 2016, lakini imeleta mageuzi muhimu ili kukabiliana na changamoto na fursa mpya zinazoibuka katika sekta hiyo. “Serikali inatambua kuwa sekta ya madini ina uwezo mkubwa wa kuchangia maendeleo ya uchumi, na sera hii inaweka mwongozo

wa kufanikisha dira hiyo,” alisema Kirui. Mkutano huo uliwakutanisha wachimbaji wa madini, wawekezaji, wawakilishi wa jamii na maafisa wa Idara ya Serikali ya Madini kujadili rasimu ya sera hiyo na kutoa maoni kabla ya kupitishwa rasmi. Sera inayopendekezwa, yenye kaulimbiu Kubadilisha Maisha kupitia Maendeleo Endelevu na Matumizi ya Rasilimali za Madini, imeainisha maeneo nane ya kipaumbele ambayo ni: mfumo wa sera na sheria; hazina ya rasilimali za madini; usimamizi wa madini na uchimbaji; uongezaji thamani na uchakataji wa madini; uchimbaji mdogo wa madini; uhamasishaji na masoko ya madini; vichocheo vya maendeleo na uendeleu wa sekta; pamoja na masuala mapya yanayogusa sekta mbalimbali. Moja ya vipengele muhimu vya sera hiyo ni kurasimisha na kuunganisha uchimbaji mdogo wa madini katika uchumi rasmi kupitia mifumo itakayoboaa usalama, kuongeza uzalishaji na kuboresha kipato cha wachimbaji wadogo. Mkaguzi wa Madini Jeff Muchiri alisema sera hiyo inaweka msisitizo mkubwa katika kuongeza thamani ya madini na kuyachakata nchini, akibainisha kuwa kwa muda mrefu Kenya imekuwa ikiuza madini ghafi nje ya nchi na kunufaika kidogo. “Kwa sasa Kenya husafirisha nje sehemu kubwa ya madini yake yakiwa ghafi,



- Mwonekano wa kiwanda cha kwanza cha kusafisha dhahabu nchini, cha thamani ya Sh5.8b kikijengwa eneo la Iguhu katika Ikolomani, Kaunti ya Kakamega. Kituo hicho kinatarajiwa kuongeza thamani ya madini na kuondoa madalali katika biashara ya dhahabu.**
- Mchimbaji mdogo wa madini akishuka ndani ya mgodi wa dhahabu Rosterman, Kaunti ya Kakamega, huku Kenya ikiendeleza mageuzi yanayolenga kurasimisha sekta ya uchimbaji madini.**

jambo linaloifanya kupata mapato madogo katika soko la kimataifa. Serikali

imejitolea kubadili hali hiyo kwa kuhimiza uchakataji na uongezaji thamani wa madini hapa nchini ili kuzalisha ajira na kuhakikisha thamani ya madini inanufaisha taifa,” alisema Muchiri. Aliongeza kuwa Kenya haiwezi kuendelea kuuza madini ghafi huku mataifa mengine yakin-ufaika na uongezaji thamani, akisema mfumo mpya wa sera unalenga kurekebisha hali hiyo. Moja ya mambo makuu yaliyomo katika sera hiyo ni kutangazwa rasmi kwenye Gazeti la Serikali kwa madini 14 ya kimkakati yanayoonekana kuwa muhimu kwa sekta mbalimbali za viwanda, zikiwemo nishati jadidifu, utengenezaji wa magari ya

umeme na teknolojia za kisasa. Serikali inasema kuweka kipaumbele kwa madini hayo kutaiwezesha Kenya kujijengea nafasi kama kitovu cha kikanda cha utafutaji, uchakataji na uongezaji thamani wa madini. Mkutano huo pia ulifahamishwa kuwa serikali imekamiliha utafiti wa kitaifa wa kijiolojia kwa kutumia ndege uliohusisha eneo lote la nchi kavu nchini Kenya. Utafiti huo ulibaini maeneo 970 yenye viashiria vya uwezo wa madini, ambayo sasa yatafanyiwa uchunguzi wa kina ardhini ili kuthibitisha uwezo wa madini na kutoa taarifa sahihi za kijiolojia kwa wawekezaji. Afisa Mkuu wa Madini wa Kaunti ya Busia, Brian Bundi, aliwataka wadau kutoa maoni yenye kujenga, akisema ushiriki wa umma utachangia kuunda sera ya mwisho. “Hii ni fursa yenu ya kusiikika. Serikali imeandaa sera hii kwa njia ya mashauriano, na tunataka kuhakikisha kuwa inaakisi matarajio ya wadau wote,” alisema Bundi.

MAKALA: UHIFADHI

Ndani ya mapinduzi ya uchumi wa kibiojia barani Ulaya na yale Kenya inaweza kujifunza



PROF. SHUKAT ABDULRAZAK

AKadri dunia inavyoendelea kutafuta njia endelevu za kukuza uchumi, uchumi wa kibaolojia (bioeconomy) unaibuka kwa kasi kama moja ya fursa muhimu zaidi za maendeleo katika karne ya 21. Huu ni uchumi unaotegemea rasilimali za kibaolojia zinazoweza kurejelezwa, ambazo hubadilishwa kupitia sayansi, utafiti, teknolojia na ubunifu kuwa chakula, dawa, malighafi za viwandani, kemikali, nishati na suluhisho za mazingira. Tofauti na uchumi wa jadi unaotegemea uchimbaji wa rasilimali, uchumi wa kibaolojia ni wa urejeshaji, wa mzunguko na unaongozwa na maarifa, hivyo kuunda utajiri huku ukilinda mifumo ya ikolojia na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Thamani ya uchumi wa kibaolojia duniani inakadiriwa kufikia dola za Marekani trilioni 4. Wakati huo huo, Afrika inamiliki moja ya hazina kubwa zaidi za rasilimali za kibaolojia duniani, ikiwa na takriban asilimia 60 ya ardhi inayofaa kwa kilimo ambayo bado haijalimwa, jambo linaloonyesha uwezo mkubwa uliopo. Ziara yangu ya hivi kar-

ibuni katika Chuo Kikuu cha Hohenheim nchini Ujerumani ilinipa taswira ya kuvutia ya jinsi mustakabali unavyoweza kuwa. Chuo hicho ni mfano wa Kituo Jumuishi cha Bioeconomy cha Kilimo, Chakula na Afya kinachounganisha kilimo, bioteknolojia, jenomiki, sayansi ya afya, uhandisi na teknolojia za kidijitali katika mfumo mmoja wa ubunifu. Mbinu hii ya taaluma mbalimbali husaidia kutatua changamoto kubwa zinazoikabili jamii. Kilichonivutia zaidi ni viwanda vya kisasa vya kuchakata mazao vilivyopo mashambani (modular on-farm biorefineries), ambapo mabaki ya mazao ya kilimo hubadilishwa kuwa protini, vifaa vya kibayolojia, nishati mbadala, biochar, mbolea na kemikali za viwandani. Hali hii huwafanya wakulima kuwa washiriki wa moja kwa moja katika kuongeza thamani ya mazao yao badala ya kuwa wasambazaji wa malighafi pekee, hivyo kuongeza kipato cha vijijini huku ikipunguza upotevu kupitia mifumo ya uzalishaji wa mzunguko. Kenya ina angalau vyuo vikuu 18 vinavyotoa kozi za kilimo ambavyo vinaweza kulengwa kwa kutumia mbinu ya vikundi (cluster approach). Mbinu hii jumuishi inaendana na dira pana ya Umoja wa Ulaya, ambapo uchumi wa kibaolojia umekuwa nguzo muhimu wa Mpango wa Kijani wa Ulaya (European Green Deal) na ushindani wa viwanda. Kupitia Horizon Europe, Circular Bio-based Europe Joint Undertaking na mifumo mingine ya ufadhili, Ulaya inawekeza mabilioni ya euro katika bioteknolojia, uzalishaji wa bidhaa za kibaolojia, mifumo endelevu ya chakula na viwanda vya mzunguko. Uwekezaji huu unachochea

ukuaji wa viwanda vya thamani ya juu, ajira bora na suluhisho rafiki kwa mazingira huku ukipunguza utegemezi wa rasilimali za mafuta. Afrika pia ina mipango kama Mpango wa Biosayansi wa Afrika na Mkakati wa Bioeconomy, ambayo inahitaji kuimarishwa na kutekelezwa kikamilifu. Afrika ina baadhi ya rasilimali tajiri zaidi za kibaolojia duniani, bioanuwai ya kipekee na idadi kubwa ya vijana wanasayansi. Hata hivyo, bara hili bado linaendelea kuuza nje mazao ghafi ya kilimo na kuagiza bidhaa zilizokamilika kwa gharama kubwa. Hatua inayofuata ya maendeleo ya Afrika lazima izingatie kuongeza thamani ya rasilimali za kibaolojia kupitia sayansi, ubunifu na ukuaji wa viwanda. Kwa Kenya, uchumi wa kibaolojia haupaswi kuishia kwenye sekta ya kilimo pekee. Unapaswa kujumuisha bioteknolojia ya kuboresha mazao na mifugo, jenomiki na uzalishaji wa kisasa (precision breeding), biosensa za ufuatiliaji wa magonjwa na usalama wa chakula, baiolojia sintetiki, bioinformatiki, mifumo ya biosecurity dhidi ya vitisho vipya vya kibaolojia, mifumo ya biosafety kwa ubunifu unaowajibika, dawa za kibaolojia, chanjo, vimeng'anya vya viwandani, kemikali zinazotokana na rasilimali za kibaolojia, malighafi mbadala, teknolojia za kubadili taka kuwa utajiri na matumizi endelevu ya

rasilimali za kibaolojia za baharini. Hizi ndizo sekta zitakazobainisha ushindani na uimara wa uchumi katika siku zijazo. Aidha, tunapaswa kujenga ushirikiano imara na sekta binafsi ili kuimarisha uzalishaji wa ndani wa bidhaa mbalimbali za afya. Uchumi wa kibaolojia wenye mafanikio hauwezi kujengwa kupitia miradi ya utafiti inayofanyika kwa kutengana. Unahitaji mbinu ya Changa-moto Kubwa (Grand Challenge) inayowaleta pamoja serikali, vyuo vikuu, taasisi za utafiti, sekta binafsi, wakulima, wawekezaji na washirika wa maendeleo chini ya vipaumbele vya kitaifa vilivyobainishwa wazi. Uzoefu wa kimataifa unaonyesha kuwa tafiti zinazongozwa na malengo maalum huharakisha ubunifu kwa kuelekeza uwezo wa kisayansi katika kutatua changamoto kubwa za jamii. Idara ya Serikali ya Sayansi, Utafiti na Ubunifu, kupitia National Research Fund kwa ushirikiano na Science Foundation for Africa, inapanga kuzindua mpango huo. Programu kama hizi zitawezesha timu za taaluma mbalimbali kuhirikiana, kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi na kuhakikisha kuwa utafiti unazalisha matokeo yenye manufaa ya kijamii na kiuchumi. Msingi muhimu wa mageuzi haya tayari umewekwa kupitia Mradi wa Bio-KE (Bioeconomy Education and Policy for Kenya). Mradi huu unaimarisha elimu ya juu, uwezo wa utafiti, ujasiriamali na utungaji wa sera ili kuharakisha mpito wa Kenya kuelekea uchumi wa kibaolojia unaotegemea maarifa. Hatua inayofuata inapaswa kuupanua Bio-KE kuwa jukwaa la kitaifa la ubunifu linalounganisha vyuo vikuu, taasisi za utafiti,

National Research Fund, serikali za kaunti na sekta binafsi kupitia vikundi vya ubunifu vya kissekta na maabara hai (living laboratories). Kwa kuiga mfano wa Hohenheim, majukwaa haya yanaweza kuanzisha viwanda vya majaribio vya kuchakata mazao, vituo vya bioteknolojia, vituo vya jenomiki, maabara za biosensa, vituo vya biosafety na biosecurity pamoja na vituo vya kulea kampuni changa ili kubadilisha uvumbuzi wa kisayansi kuwa bidhaa za kibishara na biashara zinazostawi. Ufadhili unasalika kuwa nguzo muhimu ya mafanikio. Uwekezaji wa serikali katika sayansi, utafiti na ubunifu unapaswa kuongezwa nguvu kupitia ushirikiano madhubuti kati ya sekta ya umma na binafsi pamoja na kuongeza ushiriki wa sekta binafsi. Washirika wa kimataifa kama Gates Foundation, Wellcome Trust, Umoja wa Ulaya, Benki ya Maendeleo ya Afrika, Benki ya Dunia, vituo vya CGIAR na mashirika mengine ya hisani wamekuwa na mchango mkubwa katika kuimarisha tafiti za afya, kilimo na bioteknolojia barani Afrika. Hatua inayofuata inapaswa kuwa uwekezaji wa pamoja katika majukwaa jumuishi ya bioeconomy yanayounganisha ugunduzi wa kisayansi, ubunifu, biashara na ukuaji wa viwanda. Vyuo vikuu na taasisi za utafiti lazima viwe injini za mabadiliko ya kiuchumi badala ya kuwa wazalishaji wa machapisho ya kitaaluma pekee.

Mwandishi ni Katibu, Idara ya Serikali ya Sayansi, Utafiti na Ubunifu.

“Ulaya inawekeza mabilioni ya euro katika bioteknolojia, uzalishaji wa kibiojia, mifumo endelevu ya chakula

Kenya yalenga nafasi za kazi 2m kupitia mpango wa kilimo wa Sh1.08 trilioni

NA WANGARI NDIRANGU (KNA)

Serikali imezindua Mpango wa Kitaifa wa Uwekezaji katika Mifumo ya Chakula na Kilimo (NASIP) 2026-2030. Mpango huo wenye thamani ya Shilingi trilioni 1.081 unatarajiwa kuleta mageuzi katika sekta ya kilimo, kuimarisha usalama wa chakula, kuzalisha zaidi ya ajira milioni mbili, na kuvutia uwekezaji wa sekta binafsi katika mfumo wa chakula na kilimo nchini. Akizungumza wakati wa un-

guzi wa Mkutano wa Financing Agrifood Systems Sustainably (FINAS) 2026 katika Kituo cha Kimataifa cha Mikutano cha Kenyatta (KICC) jijini Nairobi, Waziri wa Kilimo na Maendeleo ya Mifugo, Mutahi Kagwe, alisema mpango huo unaashiria mwelikeo mpya wa kufadhili kilimo kama sekta yenye ushindani na inayovutia uwekezaji. Katika hotuba iliyosomwa kwa niaba yake na Katibu Mkuu wa Idara ya Mifugo, Jonathan Mueke, Kagwe alisema NASIP ni mfumo kamili wa uwekezaji uliokadiriwa gharama zake, unaojumuisha



Katibu wa Mifugo, Jonathan Mueke, azindua rasmi Mpango wa Kitaifa wa Uwekezaji katika Mifumo ya Kilimo na Chakula (NASIP) wa mwaka 2026-2030. Kando yake ni Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Shirika la Fedha za Kilimo (AFC) nchini, Mhandisi John M. Mruttu.

sekta za mazao, mifugo, uvuvi, umwagiliaji, ukuzaji wa viwanda vya mazao ya kilimo, kilimo kidijitali, ustahimilivu dhidi ya mabadiliko ya tabianchi, utafiti, ubunifu na ufadhili wa kilimo. Waziri huyo alisema Serikali ya Kitaifa pamoja na serikali za kaunti zitachangia asilimia 35 ya gharama za utekelezaji wa mpango huo, huku sekta binafsi ikitarajiwa kuchangia asilimia 45, na washirika wa maendeleo wakichangia asilimia 20 iliyosalika. “NASIP si mpango wa kufadhili kilimo pekee. Ni mpango wa kufadhili mustakabali wa Kenya kwa kujenga mifumo imara ya chakula, kuunda ajira, kuongeza mapato ya wakulima, na kuiweka Kenya katika nafasi ya kuwa kitovu cha kikanda cha uwekezaji endelevu katika sekta ya chakula na kilimo,” alisema Kagwe.

Wafugaji wapokea Sh655milioni kutokana na malipo ya kaboni

NA DAVID NDURO (KNA)

Jamii za wafugaji kutoka kaunti nne za kaskazini mwa Kenya zimepokea Sh655 milioni kutokana na mapato ya mikopo ya kaboni kupitia mpango unaongozwa na jamii wa kuhifadhi maeneo ya malisho. Walionufaika ni wanachama wa hifadhi za wanyamapori zinazomilikiwa na jamii katika kaunti za Isiolo, Marsabit, Samburu na Laikipia, kwa ushirikiano na shirika la Northern Rangelands Trust (NRT). Fedha hizo zilitolewa kupitia Mradi wa Mikopo ya Kaboni wa Nyanda za Malisho za Kaskazini mwa Kenya (Northern Kenya Rangelands Carbon Project - NKRCP), unaogawamapato yatokanayo na mikopo ya kaboni kwa hifadhi zinazoshiriki katika mpango huo. Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi hundi hizo mjini Isiolo, Afisa Mkuu wa Uendeshaji wa NRT, Osman Hussein, aliyemwakilisha Mkurugenzi Mkuu Vimal Shah, alisema karibu asilimia 60 ya fedha hizo zitalipwa moja kwa moja kwa makundi maalumu ya jamii ndani ya hifadhi hizo. Alisema asilimia 40 iliyo-salia itagawanywa kwa usawa kati ya shughuli za uhifadhi na usimamizi wa maeneo ya malisho pamoja na kugharimia shughuli za uendeshaji wa hifadhi hizo.



Uwasilishaji wa mfano wa hundi kwa jamii za wafugaji kutoka kaunti nne kaskazini mwa Kenya ambao wamepokea Sh 655m kama mapato ya mikopo ya kaboni chini ya mpango wa uhifadhi wa nyanda za malisho unaongozwa na jamii.

Hussein alisema kuwa tangu mwaka 2022, hifadhi za jamii katika kaunti hizo zimepokea zaidi ya Sh3 bilioni kutokana na mapato ya mikopo ya kaboni. Mwenyekiti wa Bodi ya NKRCP, Andrew Dakhole, alisema hundi hizo zilizo-pokelewa kwa niaba ya jamii zinawakilisha mapato yaliyotokana na juhudi za kulinda na kurejesha maeneo ya malisho. Aliongeza kuwa hatua za jamii hizo za kuhifadhi mazingira zimechangia pakubwa kupunguza utoaji wa hewa ya kaboni angani. Ingawa mpango wa mikopo ya kaboni ulianzishwa mwaka 2013, jamii zinazoshiriki zilianza kupokea mapato ya kifedha mwaka 2022. Kwa mujibu wa Dakhole,

mpango huo ulikumbwa na changamoto mwaka jana baada ya Verra, shirika linalosimamia viwango vya kimataifa vya hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na maendeleo endelevu, kusitisha utoaji wa mikopo ya kaboni kutokana na wasiwasi kuhusu utawala, uwajibikaji na uwazi katika usimamizi wa fedha. "Hatukuweza kuuza mikopo yetu ya kaboni kuanzia Januari mwaka jana kutokana na kusitishwa huko. Hata hivyo, baada ya uchun-

guzi wa kina na kufanyika kwa mageuzi ya kiutawala, tumeruhusiwa tena kushiriki katika soko la mikopo ya kaboni," alisema Dakhole. Kwa sasa hifadhi hizo zinapitia kipindi cha mpito cha miaka mitatu ili ziweze kujisimamia kikamilifu katika uendeshaji wa mradi wa mikopo ya kaboni, huku NRT ikiendelea kutoa usaidizi wa kiufundi na kujenga uwezo wa jamii husika katika kipindi hicho. Mapema mwaka huu, NRT ilianza kuoanisha shughuli za hifadhi hizo na sheria za Kenya kuhusu soko la kaboni kwa kuhamisha usimamizi wa mradi huo kwa Kampuni Maalumu ya Jamii (Special Purpose Vehicle - SPV), muundo wa kisheria utakosimamia mpango huo kwa kujitegemea.

Hatukuweza kuuza mikopo yetu ya kaboni tangu Januari mwaka jana kutokana na kusimamishwa huko

LBDA yavuna mpunga katika kinamasi Ondago

NA SITNA OMAR (KNA)

Mamlaka ya Maendeleo ya Bonde la Ziwa (LBDA) imevuna mpunga kwa maraya kwanza katika Bwawa la Ondago, eneo la Bunge la Karachuonyo, hatua inayotajwa kuwa mafanikio makubwa katika juhudi za kuongeza uzalishaji wa mchele nchini na kupunguza utegemezi wa uagizaji kutoka nje. Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mavuno hayo,

Mkurugenzi Mkuu wa LBDA, Wycliffe Ochiaga, alisema mamlaka hiyo ilianza kulima mpunga katika eneo hilo takriban miezi mitano iliyopita na sasa imefanikiwa kuvuna mazao yake ya kwanza. Zaidi ya ekari 200 za mpunga ziko tayari kuvunwa, huku zaidi ya ekari 5,000 zikiwa tayari zimewekwa chini ya uzalishaji katika Mpango wa Umwagiliaji wa Kimira-Oluch. Ochiaga alisema mamlaka hiyo inapanga kupanua



Mamlaka ya Maendeleo ya Bonde la Ziwa yazindua uvunaji wa mpunga katika kinamasi cha Ondago.

kilimo hicho hadi zaidi ya ekari 20,000 katika kipindi cha mwaka mmoja ujao mara tu mpango wa umwagiliaji utakapokuwa ukifanya kazi kikamilifu. "Mpango wa Umwagiliaji wa Kimira-Oluch una uwezo mkubwa wa kuweka zaidi ya ekari 20,000 chini ya kilimo cha mpunga. Kwa wastani wa mavuno ya tani kati ya 3.5 na 4 kwa ekari, mradi

huu utaongeza pakubwa uzalishaji wa mchele nchini na kusaidia kupunguza pengo kati ya mahitaji ya ndani na mchele unaoagizwa kutoka nje," alisema. Alisema mpunga haujawahi kulimwa katika Bwawa la Ondago hapo awali, hivyo mradi huo unakuwa hatua ya kwanza ya kilimo cha kibishara cha mpunga katika eneo hilo.

KWA UFUPI

KEMRI yaimarisha utayari dhidi ya Ebola katika mpaka

NA ELIZABETH AKINYI NA JANE KEFRICA

Taasisi ya Utafiti wa Tiba Kenya (KEMRI) imetoa vifaa vya kujikinga binafsi (PPE) kwa Kituo cha Pamoja cha Mpakani cha Malaba (One Stop Border Post) na Hospitali ya Kaunti Ndogo ya Korcholia ili kuimarisha utayari na kuzuia kusambaa kwa virusi vya Ebola. Vifaa hivyo ni pamoja na aproni, ngao za uso, barakoa za N95, barakoa za upasuaji, buti za mpira, vipimajoto visivyogusana (thermoguns), mahema na vifaa vingine muhimu vya uchunguzi, kutenga washukiwa wa awali na ukusanyaji wa sampuli. Malaba ni mojawapo ya vituo vikuu vya mpakani nchini Kenya katika Ukanda wa Northern Corridor, kinachohudumia maelfu wa wafanyabiashara, madereva wa malori na wasafiri wengine wanaovuka kwenda Uganda kabla ya kuelekea mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC). Hali hiyo inafanya eneo hilo kuwa muhimu katika ufuatiliaji wa magonjwa na kuimarisha

usalama wa afya mipakani. Kwa mujibu wa Afisa wa Afya wa Bandari ya Malaba, Dkt Everlyne Walela, zaidi ya watu 1,500 huvuka mpaka huo kila siku, wakiwemo takriban wasafiri 800 wa kimataifa na wasafiri wa ndani wapa-tao 700. Alisema idadi hiyo kubwa ya watu wanaovuka mpaka inaongeza hatari ya kusambaa kwa Ebola kufuatia visa vilivyoripotiwa nchini DRC. Hata hivyo, alibainisha kuwa maafisa wa afya wameimarisha uchunguzi mpakani, huku msaada wa KEMRI ukiongeza pakubwa uwezo wa nchi kujitayarisha kukabiliana na ugonjwa huo. "Dekalu lililowekwa katika Kituo cha Pamoja cha Mpakani cha Malaba litatumika kama eneo la muda la kuwahifadhi watu wanaoshukiwa kuwa na Ebola kabla ya kuhamishiwa Hospitali ya Kaunti Ndogo ya Alupe kwa matibabu na uangalizi zaidi," alisema Dkt Walela. Aliwataka wakazi na wasafiri kuendelea kuwa waangalifu hadi mlipuko huo utakapokuwa umetanzwa rasmi kumalizika, akibainisha kuwa DRC bado inapambana na ugonjwa huo.

Hatimaye maji safi yafikia familia 1,000 Taita Taveta

NA ARNOLD MASILA

Zaidi ya wanafunzi 500 na zaidi ya kaya 1,000 katika eneo la Riata, Kaunti ya Taita Taveta, wanatarajiwa kunufaika na upatikanaji bora wa maji safi na salama kufuatia uzinduzi wa Mradi wa Maji wa Riata Kubwa wenye thamani ya Sh21 milioni. Mradi huo umetekelezwa na Serikali ya Kaunti ya Taita Taveta kwa ushirikiano na World Vision. Mradi huo unaotumia nishati jadidifu ya jua unatarajiwa kuboresha elimu, afya ya umma, usafi na maisha ya wakazi kwa kumaliza tatizo la muda mrefu la uhaba wa maji lililowalazimu wakazi na wanafunzi kutembea umbali mrefu kuyatafuta. Utekelezaji wa mradi huo ulifanyika kwa awamu mbili na ulijumuisha uchimbaji wa kisima kirefu, usakinishaji na uwekaji wa vifaa vya kusukuma maji, matumizi ya nishati ya jua katika mfumo wa usambazaji wa maji, upimaji wa

uwezo wa kisima, ujenzi wa tanki la maji lenye uwezo wa kuhifadhi lita 100,000, ujenzi wa vituo vinne vya maji kwa matumizi ya jamii pamoja na ulazaji wa bomba la kilomita sita kusambaza maji kwa kaya, shule na taasisi za umma. Akizungumza wakati wa uzinduzi wa mradi huo katika Shule ya Msingi ya Riata, Gavana Andrew Mwadime alisema mradi huo unaonyesha dhamira ya utawala wake ya kupanua upatikanaji wa maji safi na salama kote katika kaunti hiyo. Alisema upatikanaji wa maji ya uhakika utapunguza kwa kiasi kikubwa mzigo kwa familia na wakati huohuo kuboresha uandikishaji na mahudhuro ya wanafunzi shuleni, akibainisha kuwa awali wanafunzi wengi walikosa masomo kwa kutumia saa nyingi kutafuta maji. "Mradi wa Maji wa Riata Kubwa utapunguza kwa kiasi kikubwa umbali ambao wakazi hulazimika kutembea kutafuta maji.